

MSIKIENI YEYE



Asante, Ndugu Borders.

Habari za jioni, marafiki. Mnaweza kuketi.

² Hakika ni vizuri kurudi, usiku wa leo, huku Spokane, Washington, ambako tulifurahia ushirika mzuri sana kwenye Neno la Mungu, katika nyakati zilizopita. Nami nilikuwa tu... nilikutana na mchungaji wenu, naye alikuwa akiniambia ya kwamba hili ndilo jengo lile lile tulilokuwamo yapata miaka kumi na mitano iliyopita, tulipopitia hapa. Na hakika limebadilika na, likawa bora zaidi, nasi tunashukuru kwa hilo.

³ Nasi tunawaletea salamu kutoka sehemu zingine za dunia, za wasafiri, ambao wanasafiri kama ninyi, wakikutazamia kuja kwa Bwana. Tunaamini ya kwamba ile siku inakaribia. Sijui itakuwa ni muda gani, na kama hatakuwa hapa leo, nitakuwa nikimtazamia kesho, kama ninaishi, nikingojea tu na kutazamia wakati huo; tumekuwa hivyo, kwa miaka mingi.

⁴ Na siku moja kukesha kwetu kutakwisha, kwa kuwa tuko kama Ibrahimu alivyokuwa, wa kale, "Tunautazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu." Na kwa hiyo, tunakiri ya kwamba sisi si wa ulimwengu, tumekuwa wasafiri, tunautafuta Mji huo. Haki zetu zote za ulimwengu huu, mambo ambayo wakati mmoja tuliyathamini na kuwazia yalikuwa makuu sana, kama vile hazina za maisha, kama vile pesa na umaarufu, na, loo, mambo ambayo asiyeamini anatafuta, basi tunaweka hilo kando tunapompata Kristo, Naye anakuwa Nguzo yetu Kuu, ni Kristo, Mwana wa Mungu.

⁵ Nina furaha kuwa pamoja na kanisa hili...katika kanisa hili, usiku wa leo. Nalipenda lile bango, *Biblia Iliyofunguliwa*, hilo linamaanisha, "Ichukue yote." Hivyo ndivyo inavyotubidi kuichukua, *yote*. Ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ndilo Kigezo ambacho Mungu atauhukumu ulimwengu kwacho, ni kwa Neno.

⁶ Natoka katika eneo la Ukatoliki, kama nyote mjuavyo. Nilikuwa mvulana mdogo...Mama na baba yangu wote walifunga ndoa nje ya kanisa. Nao...Nilikuwa na wito huo maishani mwangu, tangu utotoni; natumaini mmesoma vile vitabu. Nilijua kulikuwako na Mungu, nilikuwa nimekutana Naye, alikuwa amenena nami. Na ingawa watu wangu, walidhani labda nilikuwa tu nimeshikwa na fadhaa, na kitu fulani kibaya, nimefadhaika, lakini ni—nilijua kulikuwa na Mtu, ambaye alikuwa...nilikuwa nimezungumza Naye, Naye alikuwa amezungumza nami na kuniambia nisinywe pombe, wala kuvuta sigara, wala kuuchafua mwili wangu, kulikuwa na kazi nitakayofanya.

⁷ Nami nilitaka kujua hiyo ilikuwa ni nini wakati nilipokuwa na umri wa kama miaka ishirini, kumi na minane, ishirini, nami nikaenda kanisani, akaniambia ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa. Vema basi, kama ndivyo ilivyo, basi kuna yapata madhehebu mia tisa mbalimbali yao, kwa hiyo sasa, atauhukumu kwa lipi? Hivyo basi, nikawazia, “Kama akiuhukumu kwa kanisa Katoliki, la Kilutheri hakika liko nje. Kama akiuhukumu kwa la Kilutheri, la Kibaptisti liko nje. Akiuhukumu kwa—kwa Wamethodisti, basi Wabaptisti pia, wako nje.” Nami ni—nikashangaa tu kwamba yote yalihusu nini.

⁸ Kwa hiyo, hatimaye, nikaja kugundua kwamba Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Neno Lake. Hilo Ndilo alilompa mwanadamu hapo mwanzo, kumkinga mwanadamu na dhambi, ilikuwa ni kutoa Neno, na kutokuamini tu sehemu Yake moja ni kutengwa Milele na Mungu. Hilo ndilo lililotukia wakati Hawa, kamwe hakulikataa, alitoa tu hoja kwa kitu kilicho kinyume Chake. Basi si lazima akose kuliadini, kulihoji tu. Na chochote kinachotoa hoja dhidi ya Neno, kumbuka, ni adui, usikisikilize hata kidogo; lazime iwe ni Neno.

⁹ Leo, tunaona mahali petu, makanisa, madhehebu yetu, na kadhalika, yameanza kudhoofika tena, baada ya uamsho huu mkuu imetubidi tu kwenda kote nchini. Tunaona, ya kwamba mle ndani, wa—wao wanaongeza kidogo *Hapa*, ama wachambue kidogo *hapa*, ama kitu fulani *hapa*. Hilo kamwe haliwezi kufaulu, kamwe halitafanikiwa. Ni...Mungu asingeliruhusu litende kazi hapo kwanza.

¹⁰ Basi kumbukeni tu, ya kwamba kila mgonjwa, anayeketi hapa usiku wa leo, unajua sababu ya wewe kuwa hapa, sababu ya wewe kuwa mgonjwa, ni kwa sababu mtu mmoja alikosa kuamini tu moja dogo...nusu ya sentensi ya Neno la Mungu. Neno moja tu, lilifasiriwa tu vibaya, hilo ndilo lililokufanya uwe mgonjwa; hilo ndilo lililosababisha kila makaburi huku nje; hilo ndilo lililosababisha uzee wote; hilo ndilo lililosababisha watoto wote waliozaliwa kabla ya wakati, waliokufa; hilo ndilo lililosababisha mauti yote, ilikuwa ni mtu kutokuamini tu Neno, dogo tu sana. Na kama lilisababisha huzuni hii yote, bila shaka hatutarudi nyuma katika kutokuamini tena hata sehemu Yake ndogo tu, hatuna budi kulichukua lote, kila sehemu Yake. Na hivyo ndivyo Mungu alivyoliandika, hivyo ndivyo ninavyoliadini.

¹¹ Sasa, huenda nisiwe na imani ya kutosha kulifanya lote litende kazi, lakini hakika sitasimama katika—katika njia ya mtu aliye na imani hiyo. Mara nyingi nimesema laiti ningalikuwa na imani kama aliyokuwa nayo Henoko, alitembea kidogo alasiri moja kisha akaenda zake Nyumbani pamoja na Mungu, hata haikumbidi kufa. Ningependa kuwa na imani ya namna hiyo, lakini kama sina, bila shaka ninaiombea, kwamba nitakuwa na hiyo. Nami ninaadini Kanisa linaingia mahali hapo, Kanisa te—

teule la Mungu linaingia mahali hapo, kwenye imani hiyo kuu, inayotamalaki.

¹² Sasa, ndiyo kwanza tumalize uamsho kote nchini, miaka kumi na mitano iliyopita. Kumekuwa na uamsho mkubwa sana ulioupiga ulimwengu, sasa unafifia Marekani, karibu umekwisha; nasi, tukirudi kutoka huduma za kimishenari na kujisikia vibaya sana baada ya kuwaambia watu, kule, kwamba uamsho kama huo umekuwa ukiendelea hapa, halafu tunauona ukififia. Bila shaka, kulingana na historia, miamsho hudumu kama miaka mitatu tu, halafu wanauamsho wanadumu kwa muda kama huo, ndipo wanaishia sifa za kile walichokuwa katika miaka hiyo mitatu. Sasa, tunaona ya kwamba uamsho, shauku ya watu imekwisha kabisa.

¹³ Sasa, mahubiri ya dakika ishirini ni muda mrefu, miaka kumi na mitano iliyopita ungeweza kukaa usiku kucha, na mchana kutwa na usiku kucha, na kuendelea tu. Nilikaa siku nane mchana na usiku bila kuondoka jukwaani, na kulikuwa na wengi mara tano mle kuliko walivyokuwa hapo ulipoanza. Lakini sasa, kitambo kidogo tu, wamechoka. Mnaona? Watu hawawezi kujizuia, ni, uamsho umekwisha.

¹⁴ Na sasa, tumerudi tu... Ninaondoka tena, kwenda ng'ambo, Januari hii ijayo, nadhani kwa ziara nyingine ya ulimwengu. Halafu huko Afrika, na India, na Japani, na Uchina, na huko chini visiwani tunaona ya kwamba kungali kuna moto unaowaka miongoni mwa watu kule, kwamba uamsho ungali unaendelea mle ndani, lakini katika nchi za uenyeji wetu umefifia.

¹⁵ Ni kusudi langu kuwatembelea marafiki zangu, wapendwa, niliwaita hivyo, huku na huko Pwani ya Magharibi, nilikuwa nikienda zangu Anchorage, Alaska. Huu ndio mkutano wangu wa nane mfululizo, na yapata siku nne na tano, sita usiku kwa mkutano. Tunaenda kutoka hapa chini, kurudi Portland, na kisha kuingia Vancouver, na kisha kujiandaa kwenda ng'ambo. Nami nilitaka kuwatembelea watu wote niliowajua wakati mmoja, huku na huko pwani hapa, miaka mingi iliyopita. Na ilikuwa ni majaliwa yangu makuu, kwa mwaliko wa mchungaji wenu, na kadhalika, ninii...na wahudumu wengine hapa, kusimama na kukutembelea kwa siku chache usiku. Nami nina hakika mtakuwa baraka kwangu.

¹⁶ Jambo moja tu nililotaka, hapa nje, wakati nilipokuwa hapa, kwamba mlikuwa na maji tofauti; sisi sote ni wagonjwa kwa maji haya mliyo nayo. Na kwa hiyo laiti mngalikuwa tu na maji tofauti kidogo, tumemetafuta kila mahali, hata hawana maji ya chemchemi, popote, humu mjini. Billy yuko huko nje sasa, mahali fulani, akijaribu kutafuta kidogo. Watoto na kadhalika.

¹⁷ Kwa hiyo tuko hapa kufanya vizuri sana, tuwezavyo, kwa msaada wa Injili ya Yesu Kristo. Nasi tunaleta... naona walileta...wameingiza wagonjwa fulani. Kwa kweli

hata sikujua kama huyu ndugu aliamini katika kuwaombea wagonjwa au la. Kamwe sikuwaambia wasambaze kadi za maombi ama chochote kile, niliingia tu. Kwa hiyo, usiku wa leo, tulifikiri tungejitambulisha tu, na kutafutana, na kuona yale Bwana atakayotufanyia.

¹⁸ Sasa, tunaamini katika kuwaombea wagonjwa, tunaamini yote ambayo Biblia inatetea. Sisi si wafuasi wa dhehebu fulani, dhehebu lolote, bali tunaamini tu Biblia. Nami ninaamini, ya kwamba katika Agano la Kale, wasomaji wa Biblia wanajua, kwamba Mungu alikuwa na njia ya kujua kama nabii alikuwa akitabiri sahihi, ama mwotaji akisimulia ndoto ya kweli. Wangeninii. . . Kama lilikuwa ni swali, walimpeleka chini hekaluni, kwenye Urimu na Thumimu. Sijui kile ninyi. . . mnaelewa ninachomaanisha ama la, ilikuwa ni kifuko cha kifuani cha Haruni, kilikuwa na yale mawe kumi na mawili.

¹⁹ Na kama nabii huyu alitabiri, haidhuru linasikika halisi jinsi gani, kama hizo nuru hazikuifanya Nuru hiyo ya kimbinguni juu ya kile kifuniko cha kifuani, hawakuipokea; haikutoka kwa Mungu. Haidhuru hiyo ndoto ilikuwa halisi jinsi gani, kama Urimu na Thumimu hazikuimulika, basi ilikuwa—ilikuwa—haikuwa sahihi. Sasa, hiyo ilikuwa katika ule—ule ukuhani wa Walawi, waliitumia hiyo.

²⁰ Sasa, ukuhani wa Walawi umekoma, nasi tunaye sasa, Kristo. Na, ila tungali tuna Urimu na Thumimu, hiyo ni *Hii*, Biblia. Haidhuru jinsi. . . Ninaamini Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Biblia, Lakini kama Yeye atafanya tu yale. . . Aliyoandika habari zake, hilo litakuwa sawa kwangu. Nita—nitafurahi sana, kudumu tu na yale Yeye aliyosema *hapa* ndani. Nami na—naamini Yeye atafanya hivyo, kama tunaweza tu kupata imani ya kuamini jambo hilo. Na jambo la kwanza ni kwa ajili ya wokovu, hilo ndilo jambo la kwanza.

²¹ Mingi ya mikutano yangu imejengwa juu ya uponyaji wa Kiungu, tunajua. . . haijawekwa msingi juu yake. Lakini sisi. . . Watu wanazungumza tu, kwa sababu. . . Sijui ni kwa nini, ninawaombea tu wagonjwa, nao wanapata afya, Mungu huyaheshimu tu, kwa namna fulani, hayo maombi. Nami nimemshukuru Mungu sana kwa ajili ya mamilioni ambao nimeona wakiponywa kwa nguvu Zake, mateso ya kila namna, na waliopagawa na pepo, na mambo ambayo ni vigumu kumfanya mtu kuyaamini, isipokuwa wangu pale kuyaona, waliokunjamana, waliopindika katika hali ya kila namna na madosari, wakamwona Mungu akiwafanya wa- . . . watu wamenyooka tu, wa kawaida.

²² Durban, Afrika Kusini, hivi majuzi, nilikuwa na mkutano kule ambako tulikuwa na karibu, nadhani, watu laki mbili, kwenye mkutano mmoja, kwenye uwanja wa mashindano ya

farasi wa Durban. Nilimwona akimchukua mvulana, pale jukwaani, siku moja, yapata siku ya pili ya ibada, na kumnyoosha mvulana huyo kuninii. . . sijapata kuona yoyo- . . . nilirudi tu nyuma na kuangalia. Hata hakuwa na akili timamu, naye akainuka namna *hiyo*, huku machozi yakitiririka kwenye tumbo lake uchi.

Ndipo kesho yake asubuhi meya wa Durban, Sidney Smith, akanipigia simu, akasema, “Nenda kwenye dirisha lako, uangalie kuelekea ufukoni mwa bahari.”

²³ Sasa, tulikuwa na makabila mengi, na ilitubidi kuwazungushia ua kote uwanjani, kwa sababu walikuwa na vita vya kikabila wao kwa wao. Ndipo nilipomaliza hilo. . . Karibu watu watano, ndio wote, waliofika jukwaani. Nami nikawaona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakimpokea Kristo kama Mwokozi wao wakati mmoja, elfu thelathini, waliandika kiasi hicho. Niliwaona wakivunja sanamu zao ardhini, ilionekana kama pulizo la vumbi lilipaa hewani kwa, loo, majengo kadhaa ya mji. Ndipo Bw. . . Ndipo nikafanya maombi, maombi ya kusanyiko, kwa ajili ya watu, nikasimama tu, jukwaani na kuomba, ndipo ilikadiriwa yapata wagonjwa elfu ishirini ama ishirini na tano kwenye machela na viti vya magurudumu wakaamka na kuondoka kwa wakati mmoja. Hiyo ni imani rahisi, waliona tu likifanywa mara moja, na hilo lilitosha; hilo lilitosha kwao.

²⁴ Basi kesho yake, Bw. Sidney Smith ni meya wa Durban, Afrika Kusini, jiji kubwa, mara tatu au nne ya ukubwa wa hili hapa, naye akasema, “Nenda kwenye dirisha lako ukaangalie ufukoni mwa bahari, utaona kitu ambacho hujawahi kuona.” Ndipo yale mabasi makubwa, ama, malori pale, yapata tu urefu wa ninii. . . mahali saa *ile* ilipo, ama mbali zaidi, vitanda vyao, vyenye urefu wa magurudumu sita na manane, nao walikuwa na yapata malori kumi na saba yaliyojaa mbao walizokuwa wakitumia kama machela, marungu waliyotembelea, vitu walivyovutwa kwavyo. Kulikuwako na mabasi kumi na saba yaliyojaa tu, yamejaa kabisa, watu wakiyafuata nyuma, waliokuwa wamelalia siku iliyotangulia, wakifuatilia nyuma wakiimba, katika lugha yao ya kienyeji, “Mambo yote yanawezekana, amini tu.”

²⁵ Loo, jamani. Ah, ni Kristo wa ajabu jinsi gani tunayemtumikia! Yeye ni mwenye upendo sana, si ajabu Yeye ndiye Mzuri kuliko wote kati ya elfu kumi, Yeye ndiye aliye Mzuri kuliko wote. Kwa hiyo tunampenda kwa moyo wetu wote, kumwona akifanya mambo hayo.

²⁶ Sasa, ni tofauti kidogo hapa, kwa sababu mnaona, hapa, watu wanakuwa zaidi sana wa kubahatisha, wagumu wa Injili. Lakini hapo, wanaininii tu. . . huwezi kuwafundisha dini ya kiakili, kwa sababu hawataipokea. Mkiwasambazia vitini, ama

kwenda kule na kuanza kuzungumza juu ya Kristo, ama mambo kama hayo, wataondoka na kuwaacha mmesimama hapo. Mnaona? Ha—hawatawasikiliza, Mwislamu, ama si hata mmoja wao, kwa sababu wana dini ya kiakili, hawana budi kuona kitu halisi, kitu fulani katika matendo, kukiona kwa macho yao wenyewe, wasimame hapo na kukiangalia, wakione kimenenwa katika Neno, kisha kitimie; hicho ndicho wanachotafuta. Mara moja namna hiyo, na ndipo yote yamekwisha, kweli wanaamini basi.

²⁷ Kwa hiyo Mungu ni Mungu tu, usiku wa leo, kadiri alivyowahi kuwa. Kama Yeye angali si vile alivyokuwa, kamwe hakuwako. Mnaona? Lakini hana budi kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli, tunamwamini namna hiyo. Tunaamini Yeye huwaponya wagonjwa, huwaokoa waliopotea, Yeye huwajaza na Roho Mtakatifu wale walio na mioyo yenye njaa na wanamngojea.

²⁸ Na jambo moja ninaloweza kusema kwa hili . . . Nami najua Kanisa hili la Open Bible Standard linaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa sababu ninamjua Ndugu DeWeese na hao wengine, ambao nimeshawafanyia mikutano, na, loo, ni wangapi wa hao ndugu wazuri!

²⁹ Ndipo na—nataka kusema hili, kwamba ukimchukua mtu asiyejua mkono wa kulia na wa kushoto, wamesimama pale, wanawake, bila nguo hata kidogo, kipande tu, hata hawajui ni nini mkono wa kulia na wa kushoto wala chochote kile, bali hebu wampokee Roho Mtakatifu, uwazungumzie, kisha waone jambo fulani likitukia, halafu waombe na kumpokea Roho Mtakatifu, wanafanya jambo lile lile mnalofanya, papa hapa, mnapompokea Roho Mtakatifu. Inaonyesha ya kwamba ni kwa ajili ya kila mtu, na ni Roho yeye yule. Wanatenda vivyo hivyo na kufanya mambo yale yale. Inaonyesha ya kwamba ni . . . Yeye ni wa ulimwengu mzima. Yeye ni Roho Mtakatifu wa Mungu, nasi tunamshukuru kwa ajili Yake, usiku wa leo, kwa ajili ya Mfariji wetu.

³⁰ Kwa kuwa mna ugonjwa, sijui kama nngeweza kutoa kidogo, kesho, nasi tutasambaza kadi za maombi, na kufanya ibada ya maombi kwa ajili ya wagonjwa. Hilo lingekuwa sawa? Je, ni sawa kwa wahudumu, wote, kila mtu? Wakati mwingine inatubidi kuangalia, ninachukua kulisema, lakini wengi wa watu wetu wa Full Gospel wanaachana na kuwaombea wagonjwa, hawakuamini tena. Na kuna ninii . . . [Ndugu fulani anatoa maoni—Mh.] Wasemaje? [“Tungali tunawaombea huku.”] Namshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo. Hilo ni jema. Vema. Bwana akipenda basi—basi, tuta—tutafanya hivyo.

³¹ Sasa, wengi sana . . . Nilifukuzwa kanisani, hapa si muda mrefu uliopita, ndipo jamaa fulani akaniambia akasema, “Chochote . . .” Nilimwomba viti vichache vipelekwe kwenye

jumba la mikutano, ambamo ilitubidi kuuhamishia huo mkutano, watu wapate kuingia. Naye akakataa kutupatia hivyo viti, kisha akasema hata asingemruhusu mtu yeyote aketi kwenye viti vyake ambaye hata anaamini katika uponyaji wa Kiungu. Hiyo ni Full Gospel pia, inadhaniwa kuwa, si Full Gospel, inadhaniwa tu kuwa, kubeba chapa hiyo.

³² Nampenda. Sasa, kabla hatujalikaribia Neno Lake, hebu na tumkaribie Mwandishi wa Neno tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi. Nahisi sote tunafahamiana. Sisi si wageni; sisi ni ndugu na dada. Ninawatakeni msiwe na wasiwasi, nawatakeni muwe...

³³ Sasa, ninyi wagonjwa, wachungaji wametupatia uhuru sasa, kwamba tunaweza kuwaomba wagonjwa. Kama ulienda kwa Mayo Brothers, kujua shida yako, unajua ungengojea muda gani? Labda ungengojea miezi miwili kupata nafasi, ndipo wangekuchukua, yapata majuma mawili kukupitisha kwenye kliniki. Ndipo ukipitia kwenye kliniki, ungejua tu, kama wangeweza kuipata, shida yako. Lakini kama utakuwa tu na subira, umwamini Kristo, na uangalie kitakachotukia, utaponywa. Siko hapa kuwadanganya, nipo hapa kuwasaidia.

³⁴ Sasa, wote humu ndani ambao wana, chini ya mkono wao, ninapowaomba kuinua, iwapo kuna haja ya kujulikana kwa Kristo, waweza tu kuinua mkono wako? Sijali ni nini, inua tu mkono wako, ukisema, moyoni mwako sasa, “Bwana, ninahitaji uponyaji, wokovu. Nina haja ya...” chochote kile, nina hakika Yeye anaona kila mahali. Sasa, hebu—hebu na tuombe.

³⁵ Baba mpendwa, tunakujia Wewe, Mwenyezi, Mungu aliyepo kila mahali, mwenye nguvu zote, asiye na kikomo, katika Jina Litoshelezalo kwa Yote la Yesu Kristo, Mwanao. Tunakuja kwa sababu Yeye alitwambia, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa.” Basi hatuna kitu kingine chochote ambacho tungetamani kukaribia kwacho, kwa sababu jina la kanisa letu, ama shirika letu, jina letu wenyewe, au jiji letu, au jamii yetu, au taifa lisingempendeza Mungu hata kidogo, bali inampendeza tunapokuja katika Jina la Mwanawe.

³⁶ Kwa hiyo tunakujia Wewe, Baba. Nasi hatutaki utuelekeze kwenye Kiti cha Hukumu, bali kwenye Kiti cha Rehema, kwa kuwa tunahitaji rehema. Sisi ni wahitaji, Bwana, Wewe unajua haja zetu. Unajua ni kitu gani kilichokuwa chini ya mkono huo ambao ndio kwanza uinuliwe, kote kwenye jengo hili, Wewe unajua walichohitaji. Niliwaona hawa wagonjwa, baadhi yao wamelemaa sana hata hawakuweza kuinua mkono wao, bali walikuwa wakijaribu kuuinua, Mungu, nina hakika Wewe uliona hilo, kwa kuwa, “Hata shomoro asingeweza kuanguka barabarani,” alisema Yesu, “bila Baba kujua.”

³⁷ Sasa, Mungu, ninakuomba rehema. Jalia kwamba kila mmoja wa mikono hiyo iliyoinuliwa, kabla ya ibada hizi

kufungwa, wikendi hii ijayo, kwamba kila haja itatimizwa. Jalia watu wawe na subira. Kumbukeni, “Wale wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya. Watapaa juu kwa mbawa kama tai.” Tunaombea u—uamsho juma hili, Bwana, kuwaka moto kwa Roho Mtakatifu mioyoni mwetu.

³⁸ Baba, kutoka kwa mchungaji, na moyo wangu, wote walio pamoja nami, na kila mshiriki wa kanisa kote kote mpaka ma—maskani ya wasokwao, na iwe, Bwana, juma hili, kwamba tutaona mambo makubwa kwa wingi sana. Roho Mtakatifu na aturehemu tu usiku baada ya usiku. Jalia tuwaone watu hawa, kila mmoja kwenye vitanda vya wagonjwa na machela, kila mmoja wao, usiku baada ya usiku, wakichukua mahali pao, wameketi kule nyuma pamoja na watu wengine, haitawabidi kuyatumia tena.

³⁹ Jalia, Bwana, kwamba kila mwenye dhambi mkaidi, mvulana, msichana, mwanamume, ama mwanamke atakuwa akiangaza kwa Roho wa Mungu moyoni mwao kabla mkutano haujaisha. Jalia kanisa hili dogo, Bwana, likue, wala si hili tu, bali kila kanisa mjini. Jalia uje uamsho wa mtindo wa kale, ambao usiwe tu ni Maonyesho ya Ulimwengu katika mji mwenzi, lakini jalia uwe ni uamsho unaotikisa ulimwengu. Huo ndio tunaotamani, Bwana, ambao utaitikisa mioyo ya watu, Bwana, ambao utawarudisha kwenye maarifa ya Bwana Yesu, na rehema na neema Yake kwa watu Wake.

⁴⁰ Sasa, Baba, hatungeomba hili isipokuwa tuwe na imani ya kuamini ya kwamba lingeweza kutendeka. Nasi tunaamini ya kwamba kwa—kwa jumla inawezekana, Bwana, na huenda ikawa, kwamba Mungu atatufanyia jambo kama hilo, nasi tunalitazamia.

⁴¹ Na sasa, Bwana, lisaidie, na ulibariki kanisa hili na mchungaji wake, halmashauri yake ya wadhamini, mashemasi, na chochote kinachohusishwa au kushirikishwa nalo, washiriki wake wote, na washiriki wote wageni, na wachungaji wote; Mungu, usiache hata mmoja wao, kuanzia aliye mdogo kuliko wote hata aliye mkubwa zaidi.

⁴² Pia jalia tuwe na uamsho mioyoni mwetu, Bwana, tukiwaka kwa Moto wa Mungu. Hatujui tumbakisha muda gani zaidi, bila shaka kuna shaka sana kwamba tutakuwa hapa kwa muda mrefu. Na, loo, ni wazo tukufu jinsi gani kujua ya kwamba maskini miili hii michafu itabadilishwa moja ya siku hizi, “katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Nasi tutanyakuliwa pamoja, kumlaki Bwana hewani.” Siku hii yenye uchovu ya maradhi, katika maskini nyumba hii ya wadudu ya dhambi, tutapaa juu kwa mbawa za tai na kuruka tuondoke moja ya siku hizi. Na hata mauti yenyewe hayatalizuia tukio hili kuu, “Kwa kuwa baragumu ya Mungu italia, waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Kisha sisi pamoja nao tutanyakuliwa ili

kumlaki.” Tunakutazamia kuja kwa siku hiyo kuu, Bwana. Tusaidie sasa.

⁴³ Na tukusudie mioyoni mwetu, usiku wa leo, kutulia mbele za Bwana, kumngojea Yeye, kungojea, dakika baada ya dakika, tukitarajia neno lifaalo kusemwa, ama jambo linalofaa kufanywa ambalo lingetupa imani ifaayo ambayo ingekimbilia moja kwa moja kwenye baraka za Mungu.

⁴⁴ Tunapoendelea kungojea, Bwana, kusoma Neno, nisaidie, Ee Mungu, kwamba nitakuwa mwaminifu sana na kupakwa mafuta kwa Roho, wabariki wahudumu wote, kwamba watakuwa vivyo hivyo, na watu wote, kwa sababu inatuhitaji sote pamoja, Bwana, kwa kuwa tumekusanyika katika Jina Lako, tuingojea katika Jina Lako, tukitarajia katika Jina Lako baraka hizi, ambazo tumeomba sasa, zitimie, tunaziweka juu ya madhabahu Yako karibu na Dhabihu ya Bwana Yesu, kwa imani yote tuliyo nayo, jalia kila mmoja wetu, haja zetu huko juu, na kuliombea katika Jina la Yesu Kristo lipate kutimia. Amina.

⁴⁵ Sasa, hebu na tuwe waaminifu sana, na wenye matumaini sasa, ya kwamba kile tulichoomba . . . Ingekuwa ni kosa kuomba jambo fulani halafu kutokuliamini. Mnaona, hatuninii—hatuna uaminifu wa kutosha kwa—kwa ibada zetu, yabidi tuwe waaminifu sana.

⁴⁶ Nami nashangaa, hivi mnaweza kusikia vizuri kwenye roshani? Sio tu . . . Naam, huko nyuma, ninauona mkono wao. [Ndugu fulani anasema, “Nilijaribu yote, usiku wa leo.”—Mh.] Ulijaribu tu, vema, ajabu. Hilo ni sawa. Sasa, simaanishi kupiga mayowe. Wakati mwingine . . . Nimezoea kuzungumza huko nje, na ninazungumza kwa sauti kubwa kidogo, kwa hiyo simaanishi kupiga kelele.

⁴⁷ Na sasa, kuwa tu wewe mwenyewe, rahisi, mnyenyekevu, ukingojea kuja kwa Bwana. Sasa, hatuamini katika madoido, kitu kinachoang’aa. Mnajua, daima nilisema, “Hollywood hung’aa, lakini Ukristo urnameka.” Kuna tofauti chungu nzima kati ya kung’aa na kumeka. Hollywood hung’aa kwa tabaka kubwa, na—na jamii, na, loo, madoido, lakini ninii . . . Ukristo humeka kwa unyenyekevu; njia ya kupanda juu sikuzote ni kushuka.

⁴⁸ Sasa, ninatumaini ya kwamba kila mtu atajazwa na Roho Mtakatifu. Na sasa, kabla ya kuweza kujazwa na Roho Mtakatifu, huna budi kufa kwa nafsi yako kwanza, kusudi uzaliwe mara ya pili.

⁴⁹ Hivi punde nimepata ajali, mngali mnaona makovu usoni mwangu, ambapo, nikipiga risasi kwa bunduki niliyopewa na mtu fulani, nayo ikalipukia usoni mwangu, Weatherby Magnum kubwa, yapata ratili elfu moja mia nane za presha, chuma zikipiga usoni mwangu na machoni mwangu. Ni ajabu hata nina macho, ni neema ya Mungu tu, na . . . ama hata kichwa

ama mabega. Na kile walichosema ndicho kilichokuwa shida, ilikuwa kwamba bunduki ilikuwa ikivuja presha. Ilikuwa ni bunduki iliyogeuzwa ambayo ilikuwa, ilifanyizwa kutoka kwa ninii, si Weatherby Magnum ya kawaida, lakini Winchester iliyobadilishwa kuwa Weatherby Magnum. Sikuzote nilitaka moja, lakini kamwe nisingeweza kuwazia ningeweza kununua moja, nisingemruhusu yeyote wa marafiki zangu kuinunua hiyo, ni ghali.

⁵⁰ Sasa, mwajua, ninawinda wanyama wakubwa, kote ulimwenguni, Afrika, India, Alaska, kila mahali. Nami hulenga shabaha mara nyingi, nami ni—nilikuwa nikijaribu bunduki hii ambayo mtu fulani alikuwa ameigeuza... alifanya Weatherby kuigeuza, lakini hawakuirekebisha vizuri kwa njia fulani, ikalipuka tena, badala ya kutoka, ililipuka tena, na mitambo yote ikayeyukia tu mikononi mwangu. Na ninii... Mtutu ukalipukia umbali wa yadi hamsini, na—nayo darubini na vipande vikagonga miti, nalo shina likarushwa yapata yadi ishirini na tano, thelathini nyuma yangu, kilichosalia kwayo, nami nilikuwa tu nimesimama pale, nikitoka tu na damu, na damu ikiruka kila mahali. Yote niliyoona ilikuwa ni moto mwekundu ukiruka juu kama darini *pale*, na hayo ndiyo yote niliyokumbuka kwa sekunde moja ama mbili.

⁵¹ Kile... Nilipata mahubiri kutoka kwake. Mnaona, bunduki hiyo haikuwa... kwa kugeuzwa kuwa kitu ambacho haikuwa, walipandisha presha. Badala ya kuirusha risasi *huko*, ililipua mtambo *hivi*. Sasa, hivyo ndivyo, inavyofanyika mtu anapomjia Mungu, na kumsalimia tu mhubiri kwa mkono ama chochote kile, wala asirudi, apate kufa na kuzaliwa mara ya pili.

⁵² Sasa, kama bunduki hiyo ingalianza, tangu mwanzo, kwenye mitambo ya Weatherby, na ilikuwa imefanywa bunduki ya Weatherby, kamwe isingelipuka. Mnaona, kwa sababu ingekuwa ni bunduki ya Weatherby, feleji yao ile ile iliyotengenezewa mitamboni mwao, na kila kitu, na kutokea moja kwa moja kuwa bunduki ya kawaida inayopaswa kuwa. Lakini kwa kuwa ilikuwa ni kitu kingine, na si tu kilichogeuzwa, bali kilipotoshwa kikawa kitu fulani, na hilo ndilo lilifanya kilipuke.

⁵³ Na hivyo ndivyo tunavyojikuta safarini. Tunaona, mara nyingi sana, ya kwamba watu hawawezi kabisa kustahimili pre—presha, ni kwa saba... ya kuwa Mkristo, ni kwa sababu kweli hawajapata kufa kwa nafsi zao, na kuzaliwa mara ya pili, wakafanyizwa kutoka kwa mitambo ya Mungu wapate kustahimili huo mzigo, presha inayokuja dhidi ya Mkristo halisi.

⁵⁴ Ukijaribu kutembea na mtakatifu halisi wa Mungu, halafu ukute kwamba presha inakupiga namna *hiyo*, utalipuka na kurudi mahali ulipokuwa kwanza kabisa. Lakini kama umezaliwa mara ya pili, na kujazwa kweli na Roho wa Mungu, basi umeshinikizwa na Mungu kustahimili presha ambayo

ulimwengu unaweza kuweka dhidi yake namna *hiyo*, lakini lazima iwe ni hivyo kwanza.

55 Sasa, nawatakeni msome pamoja nami, usiku wa leo, kutoka kwenye mlango wa 17 wa Injili ya Mathayo Mtakatifu, vifungu vya kwanza 4 au 5 kwa muktadha na somo.

Hata baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani,

Akageuka sura mbele yao: uso wake ukaangaza kama jua, na mavazi yake yakawa meupe kama . . . mwanga.

Na tazama, Musa na Eliya wakamtokea, wakizungumza naye.

Ndipo Petro akajibu, akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwa hapa: ukitaka, na tufanye hapa vibanda vitatu; kimoja chako wewe, ama kimoja cha Musa, . . . kimoja cha Eliya.

Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli: . . . na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.

56 Bwana akipenda, ninataka kuchukua kutoka kwenye hilo somo, hayo maneno matatu ya mwisho: *Msikieni Yeye* [English: *Hear Ye Him*—Mfa.]

57 Sasa, hilo ni fungu dogo sana la kuanzisha uamsho, juu ya maombi ambayo tumeomba na haja za watu. Karibu kila mkono hapa ndani ulikuwa juu, dakika chache zilizopita, kwa ajili ya maombi. Sasa, nitaamini ya kwamba Mungu atajibu kila moja la maombi hayo; aminini pamoja nami, Naye atafanya hivyo. Sasa, mnasema basi, “Ati kuchukua maneno matatu madogo kwa ajili ya somo, *Msikieni Yeye*, kwa hayo yote?” Naam. Hayo yanatosha. Mnaona, si—si ukubwa, ni thamani yake, kwa sababu ilikuwa ni Mungu akinena Mwenyewe, “*Msikieni Yeye.*”

58 Wakati mwingine ni mambo madogo tunayoacha ambayo huharibu imani ye—yetu kuu. Tutaona kitu kidogo kikija, hali ya hewa ni joto sana, walichoka sana, *hiki*, ama kitu kidogo kama hicho, ambapo u—utakwepa kuja mkutanoni tena, ama labda mtu fulani alikiuka utaratibu, kitu fulani kilienda kombo, ama kitu fulani, halafu basi, papo hapo, ndipo unaposhindwa. Unaona, kama . . .

59 Lakini unaona, imani ni halisi sana, kamwe . . . huwezi kuizuia imani; haidhuru ni nini, unaenda, utafanya hivyo kwa vyovyote vile. Haidhuru mtu mwingine yeyote anafanya nini, kama unaamini, utadumu nayo, kwa sababu imani haina kizuizi; huenda ukawa na vingi, lakini imani yako haina. Kwa hiyo itadumu, dumu tu moja kwa moja nayo.

⁶⁰ Sasa, kama vile hapa, miaka kadhaa iliyopita, kabla ya . . . Ni nini . . . ? Wakati yule Mfalme mkuu George wa Uingereza alipokuwa hai, alizuru Canada, wanasema, na kulikuwa na . . . shule zote ziliachiliwa, kule, kwa—kwa ajili ya hiyo hafla, kwa ajili ya huyo mfalme na malkia. Nao walimu wakawapa wa—watoto bendera ndogo ambazo wangeweza kushika na kumpeperushia mfalme wakati akipita, kama heshima kwa uaminifu wake, na, uaminifu wao kwake, hasa.

⁶¹ Basi mfalme akiisha kupita, watoto wote walipaswa kurudi tena, shuleni. Na katika shule *fulani*, mbona, ninaamini ilikuwa ni huko Vancouver, ambapo watoto wote walirudi ila msichana mmoja mdogo.

⁶² Vema, mwalimu alikuwa amechanganyikiwa kabisa, naye akakimbia mitaani na kuanza kumtafuta mtoto huyo mdogo. Akaangalia huku na huko mitaani, kwenye magari, ndipo akamsikia mtu akiguna, akilia kama mtoto. Naye akaangalia, amesimama nyuma ya moja ya nguzo za simu, na huyu hapa maskini yule kipenzi, amesimama kule nyuma, amebeba maskini bendera yake upande *huu*, akilia.

Ndipo mwalimu akamwambia, akasema, akamwita kwa jina, naye akasema, “Kuna nini, Kipenzi?” Naye msichana huyo mdogo hakujibu.

Naye akasema, “Kwani hukumwona mfalme?”

Akatikisa maskini kichwa chake, “Naam,” alikuwa amemwona mfalme.

Kisha kasema, “Je, ulimpeperushia mfalme bendera yako ndogo?”

“Naam,” alipata kumpeperushia mfalme bendera yake.

“Vema, basi,” akasema, “mbona unalia?”

Akasema, “Unaona, mimi ni mdogo sana, Mwalimu,” akasema, “Nilimwona mfalme, lakini mfalme hakuniona nikipeperusha bendera yangu ndogo, nilikuwa mdogo sana.”

⁶³ Hiyo huenda ikawa hivyo kwa Mfalme George, huenda hakumwona huyo msichana mdogo, lakini kuna jambo moja kumhusu Mfalme Yesu, sijali unafanya kidogo jinsi gani, Yeye atakiona. Yeye yuko tayari daima. Yeye huangalia kila hatua ndogo unayopiga, na anakupenda.

⁶⁴ Sasa, kwenye tukio hili, Mungu anakutana na watu Wake. Sasa, mara nyingi Mungu hukutana katika milki za makusanyiko makubwa; Yeye hukutana na makusanyiko madogo. Wakati mmoja alikutana na mia tano, tena, akakutana na sabini, kumi na wawili, watatu, na hata mmoja. Haidhuru kusanyiko ni dogo jinsi gani, Mungu daima atakuja unapokuwa na haja na unaamini ya kwamba Yeye atakuwako.

⁶⁵ Yesu alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa hapo katikati yao.” Sasa, hiyo ni ahadi Yake, kama hiyo si kweli, basi hakuna Mbingu, hakuna Kitu kama Mwokozi, mnaona, kama hiyo si kweli. Haina budi kuwa ni kweli.

⁶⁶ Kwa hiyo Mungu hukutana na makusanyiko makubwa, kisha anakutana na makusanyiko madogo. Haijalishi, popote tu mtu fulani ana imani, Mungu atakutana nao.

⁶⁷ Sasa, kwenye tukio hili, lilikuwa liwe ni tukio kuu. Kwa hiyo Mungu kwa kawaida huwaita watu, wakati ana jambo kuu la kuwaambia, Yeye huwaita watu Wake pamoja. Labda ni wawili tu, labda ni watano, labda ni elfu moja, lakini Yeye huwaita pamoja, wakati akiwa na kitu halisi... jambo ambalo hana budi kuliambia Kanisa Lake.

⁶⁸ Sasa, kwenye tukio hili, hapana shaka lilikuwa kubwa sana, kwa maana Petro, miaka kadhaa baadaye, aliuita “mlima mtakatifu.” Aliurejea kama “mlima mtakatifu.”

⁶⁹ Sasa, siamini ya kwamba kweli alimaanisha ya kwamba huo mlima ulikuwa mtakatifu. Si mlima mtakatifu, ilikuwa ni Mungu mtakatifu juu ya mlima mtakatifu. Si Kanisa takatifu, kama tunavyoliita Kanisa takatifu, ama watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya watu, Roho Mtakatifu ndani ya Kanisa. Sio Kanisa takatifu, Roho Mtakatifu ndani ya Kanisa, huyo ndiye anayewafanya watakatifu, kwa sababu Yeye Ndiye aliye mtakatifu.

⁷⁰ Sasa, Petro aliuita “mlima mtakatifu,” kwa sababu Mungu Mtakatifu alikuwa kwenye mlima huu. Na kabla Mungu hajafanya jambo lolote, kwa kawaida, duniani, Yeye kwa kawaida hunena habari zake kutoka Mbinguni kwanza. Uliwahi kuona jambo hilo? Daima hunena kutoka Mbinguni kwanza. Ya kimbinguni daima hujidhihirisha kisha yanashuka, na kwa watu.

⁷¹ Kama ukiangalia, kabla Israeli hawajaitwa kutoka Misri, Musa alikuwa amejaribu kufanya hivyo, akiamini ya kwamba alikuwa ndiye mtu aliyepaswa kutoa U—Ujumbe, lakini alikuwa amejaribu kufanya hivyo kwa mapenzi yake mwenyewe, kwa msimamo wa kiakili, bali kabla ya wakati ufaao. Lakini wakati ulipowadia, kulikuwa na Mgeni aliyeshuka kutoka Mbinguni, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe. Akaja kwenye kijiti kilichowaka moto, Naye akanena na Musa kabla hajatuma.

⁷² Ninaamini ya kwamba kila mtu, kabla hajatoka kwenda hudumani, kuhubiri Injili, anapaswa kwanza kupata tukio na Mungu kabla hajaenda, kwa sababu katika siku hii ya usomi, kama Biblia inavyotuambia, itakuja siku hii, “Kwa maana watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake.”

⁷³ Nao wana mabingwa wa kielimu ulimwenguni, siku hizi, ambao karibu wanaweza kueleza vinginevyo kila kitu ambacho Mungu alisema kuwa ni kweli. Wanaweza kulichukua kutoka kwenye msimamo wa kitheolojia, wa usomi. Na kama ukichukua tu nia yako mwenyewe ya kuwazia, kutoa hoja, kama Hawa alivyofanya hapo mwanzo, wanaweza kuelezea kila kitu cha Biblia kukipeleka mbali na wewe.

⁷⁴ Lakini kama mwanamume, ama mwanamke amewahi kuwa upande wa nyuma ya jangwa, katika mchanga huo mtakatifu, ambapo hakuna mwenye elimu anayeweza kusimama, na hapo akawasiliana na Mungu aliye hai, hakuna ibilisi, wala mwanasayansi, wala chochote kile kinachoweza kueleza hayo vinginevyo. Ulikuwapo, lilitukia, unajua ni kweli. Hakuna mtu anayeweza kuliondoa kwako: Ulikutana na Mungu.

⁷⁵ Nami ninaamini ya kwamba Mungu, katika kila wakati, akimtuma mjumbe kila mara, kwanza, hukutana na mtu huyo kwenye mahali patakatifu, kwa sababu haina budi kuwa hivyo, kuna uovu mwingi sana kujaribu kuelezea mambo yote ya kimbinguni vinginevyo. Na palipo na Mungu wa kimbinguni, kutakuwa na mambo ya kimbinguni yakitendeka, kwa sababu Yeye ni wa kimbinguni.

⁷⁶ Sasa, Mungu alinena kwanza, na Musa, kabla ya jambo la kimbinguni kutukia, la miujiza Yake. Na pia, Mungu alinena na Yohana Mbatizaji kabla ya kuja kwa Kristo. Daima. Kasema, “Yeye aliyeniambia, kule nyikani, ‘Yeye utakayemwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’” Mnaona?

⁷⁷ Sasa, Yohana, kweli, alitoka kwenye familia ya kuhani. Baba yake, Zakaria, alikuwa kuhani, naye alikufa wakati Yohana alipokuwa mvulana mdogo tu. Badala ya Yohana kwenda na kufuata mkondo ule ule wa mawazo ya huduma ambayo baba yake alikuwa nayo, kazi hiyo ilikuwa muhimu sana, asingeweza kuifanya hivyo, ilimbidi kwenda nyikani na kungojea kule mpaka aliposikia, kwanza, kutoka kwa Mungu, kwa sababu alikuwa ndiye angemtambulisha Masihi. Na siku hizo walikuwa na kila namna ya ishara kwa ajili ya Masihi. Walikuwa na *hili*, *lile*, ama *linginelo*, na *hili* litakuwa Ndilo.

⁷⁸ Hapana shaka Mafarisayo wangekuja, kasema, “Tunaye Dk. Jones hapa juu, yeye ni mmoja wa watu wazuri sana. Ninajua hana budi kuwa ndiye Masihi, ndivyo hivyo, kwa sababu yeye ni mtu mwerevu sana. Anaishi vizuri sana na watu, anavalia vizuri sana,” na—na kadhalika; kila mmoja angalikuwa na mtu.

⁷⁹ Kwa hiyo lakini Mungu anapojitayarisha kufanya lolote, Yeye humwita mtu fulani kando na kunena kutoka Mbinguni kwanza. Ndipo wanajua kile hasa wanachozungumzia, haiwabidi kuogopa chochote wala kuchukua chochote cha mawazo ya mtu yeyote, wanajua kinachohitajika hasa, nao

wanaenda kukichukua. Huo ndio Ujumbe ambao Mungu daima hunena kwanza.

⁸⁰ Na hapa, Mungu alikuwa anaenda kufanya jambo kubwa, kwa sababu alikuwa akiwaleta Petro, Yakobo, na Yohana. Sasa, hiyo ni, ningeliita tumaini, imani, na upendo: zile karama tatu kuu za Mungu. Tuseme, mchukue Petro kuwa imani, na Yakobo kuwa tumaini, na Yohana daima ni upendo, ambao ni upendo. Naye anachukua imani, tumaini, na upendo, kisha anapanda juu mlimani, kwa sababu anajiandaa kufanya jambo fulani, Yeye anaenda kutoa tamshi, Naye anataka lithibitishwe. Naye sikuzote hulithibitisha kwa mashahidi watatu, mashahidi wawili au watatu. Hilo lilikuwa ni tamshi la Agano la Kale. “Mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitike.”

⁸¹ Naye anapanda mlimani, akiwaita watu hawa watatu, karama tatu kuu za watu waliokuwa pamoja Naye, na kuwapandisha juu mlimani, halafu ana Viumbe watatu wa Mbinguni. Jambo fulani halina budi kutukia, Yeye anao mashahidi watatu wa duniani na Mashahidi watatu wa Mbinguni. Kuna Musa, Eliya, na Yesu aliyegeuka sura, akageuzwa; na kulikuwako na Petro, Yakobo, na Yohana; wa duniani na wa Mbinguni wote wakikutana pamoja sasa.

⁸² Na sasa, Musa na Eliya, halafu Yesu alitukuzwa mbele zao, nayo mavazi Yake yakang’aa kama jua. Sasa, Yeye alikuwa akijaribu kufanya nini hapa? Tunaona ya kwamba walipanda juu, nao wakaona Wingu limemtia uvuli, mavazi Yake yakabadilika, vazi alilokuwa amevaa, nalo likaang’aa kama jua katika mwangaza wake, nalo Wingu lilikuwa juu Yake, ndipo Sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye; msikieni Yeye.”

⁸³ Sasa, nionavyo mimi, yale aliyokuwa akifanya...Mungu kamwe hajawahi kumwomba mtu yeyote kufanya jambo lolote asilofanya Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika Uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, hata hivyo alikuwa ni Nabii, hata hivyo alikuwa ni Mwanadamu, lakini alikuwa zaidi ya hao, alikuwa ni Imanueli, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Ninaamini hilo.

⁸⁴ Hivyo ndivyo alivyokuwa hasa, kwa sababu mtu yeyote, ama nabii, ama mtu wa kawaida angezaliwa jinsi tunavyozaliwa basi tungali katika dhambi zetu. Lakini mnaona, Yeye alizaliwa na bikira. Hakuna mtu aliyekuwa na uhusiano wowote nalo ila Mungu Mwenyewe. Mungu, Muumba, alimtia uvuli bikira Mariamu, akaumba ndani yake chembechembe ya damu.

⁸⁵ Sasa, sote tunajua ya kwamba—ya kwamba uhai hutokana na jinsia ya kiume. Kama tu vile kuku anavyoweza kutaga yai, lakini kama hajawa na ndege wa kiume, kamwe halitaanguuliwa,

halijarutubishwa. Basi Jinsia ya kiume ilikuwa ni Mungu. Na ilikuwa ni u—uumbaji ambao Mungu. . .

⁸⁶ Sasa, ninyi Wakatoliki wa thamani hapa, sio kuumiza hisia zenu, bali mnaposema, “Mariamu, mama wa Mungu,” vema ni nani aliyekuwa baba wa Mungu, kama huyo alikuwa ndiye mama Yake? Mnaona? Mnaona? Yeye, siye mama wa Mungu, alikuwa ni kiangulio ambacho Mungu alitumia. Mungu alimtumia Mariamu, yeye si mwombezi, yeye ni. . . wala yeye si mpatanishi, yeye ni mwanamke ambaye Mungu, Baba, alimtia uvuli, na katika nguvu Zake za kuumba, pasipo na tamaa yoyote ya kujuana kimwili hata kidogo, aliumba ndani yake Chembe ya uhai iliyomfanya Mwana wa Mungu. Kwa hiyo, Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu.

⁸⁷ Mtu fulani alisema tuliokolewa kwa damu ya Kiyahudi, kama ndivyo tulivyo, basi ingebidi kuwe na kujuana kimwili. Kwa hiyo ni. . . Ye—Yeye alikuwa ni Damu ya Mungu, Damu iliyombwa, ambapo Mungu, Mwenyewe, alikuwa amefungwa katika maskini, Mtoto mchanga. Naye alikuwa Yehova Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, sasa, sio tu nabii.

⁸⁸ Baadhi ya watu husema, “Loo, alikuwa ni mtu mzuri.” Hadithi ndogo—ndogo: Hapa wakati fulani uliopita mwanamke mmoja aliniambia, akasema, “Bw. Branham,” akasema, “Na—napenda kukusikia, lakini,” akasema, “kuna jambo moja tu nililo nalo dhidi yako.”

⁸⁹ Nikasema, “Ikiwa kuna moja pekee, Bwana ashukuriwe.” Nikasema, “Ninafurahia hilo, kwa kawaida ni karibu kila kitu.” Nikasema, “Nawe unasema una jambo moja tu? Hebu tulisikie, Dada.” Alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo haliadini ka—katika Uungu wa Kristo. Wanaadini Yeye alikuwa ni mtu mzuri, mwalimu, nao waliadini uponyaji wa Kiungu, na kadhalika. Lakini wao—wao kamwe hawakuadini kwamba Yeye alikuwa ni Mungu.

Kisha akasema, “Unajivunia Yesu kupita kiasi.”

⁹⁰ Nikasema, “Loo, jamani. Kama hiyo ndiyo dhambi iliyo ndogo sana niliyo nayo,” nikasema, “basi ni—nitaingia vizuri.” Nikasema, “Ati na—namjivunia Yesu kupita kiasi?” Nikasema, “Dada, kama nilikuwa watu hamsini, huyu, nisingeweza kumjivunia vya kutosha, kama nilijivunia mchana na usiku. Nisingeweza kusema mengi kupita kiasi kwa ajili Yake, haidhuru ningesea nini, bado. . . ni zaidi ya hayo, ‘Nusu haijasimuliwa bado,’ baada ya kuwa imekuwa miaka elfu mbili ya kuijaribu.” Nikasema, “‘Nusu haijasimuliwa bado!’ Ungetaka nini. . .”

Akasema, “Vema, ulisema unaadini Biblia.”

Nikasema, “Naadini.”

Akasema, “Kama nitakuthibitishia, kwa Biblia yako, ya kwamba yeye hakuwa kitu ila mwanadamu,” akasema, “uta—utakubali?”

Nikasema, “Kama Biblia inasema hivyo.”

Akasema, “Vema, nitakuthibitishia ya kwamba yeye hakuwa Mungu, kama ulivyosema alikuwa.”

Nami nikasema, “Vema, ninataka kukusikia.”

⁹¹ Naye akasema, “Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, wakati Yesu alipoenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema, ‘Alilia.’” Kisha kasema, “Asingeweza kuwa Mungu na kulia.”

Nikatoa tamshi la kifidhuli kidogo, natumaini hamwazii ni kukufuru, bali nilimwambia, nikasema, “Mama, hayo ndiyo Maandiko yako?”

Akasema, “Hapo ndipo ninaposimamia.”

⁹² Nikasema, “Hiyo ni dhaifu kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Mbona, kamwe hutaninii...Hiyo ni...Mbona, humaanishi kusema jambo kama hilo. Mbona,” nikasema, “Yeye alikuwa Mungu na mwanadamu pia. Wakati alipokuwa akienda zake kwenye kaburi la Lazaro, alilia, hiyo ni kweli, hiyo ilikuwa ni sehemu Yake ya kibinadamu, lakini aliposimama pale, akayanyosha maskini mabega Yake, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku,’ naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne akasimama kwa miguu yake, na akaishi tena, niambieni mahali ambapo mwanadamu anaweza kufanya hivyo! Huyu alikuwa ni Mungu, angeweza kunena Ndani Yake.” Ilikuwa ni kweli.

⁹³ Alikuwa na njaa wakati mmoja, ya chakula, akaangalia kila mahali kwenye mti apate chakula, alikuwa na njaa, akaaulaani huo mti kwa sababu haukuwa na tini juu yake, Bali alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano, kisha wakaokota vikapu vitano vilivyojaa, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu. Hakika ndivyo.

⁹⁴ Huyu alikuwa ni Mwanadamu, usiku ule baharini, ambapo alikuwa amehubiri mpaka kinywa Chake kikakauka, nao mwili Wake ukachoka, ndipo pepo elfu kumi wa baharini wakaapa wangemzamisha, usiku huo, katika maskini meli hiyo ndogo ikirushwarushwa huku na huku kama kifuniko cha chupa, huko nje, katika dhoruba. Huyu alikuwa ni Mtu aliyekuwa amelala pale usingizi, lakini alipoamshwa, akaweka mguu Wake kwenye demani ya hicho chombo, akaangalia juu, na kusema, “Amani, tulia,” nazo pepo na mawimbi yakamtii Yeye, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu. Bila shaka alikuwa.

⁹⁵ Ilikuwa ni Mwanadamu aliyelia msalabani apate rehema, “Naona kiu. Nipe maji ninywe.” Ilikuwa ni Mwanadamu akilia

pale, lakini kwenye siku ya tatu, wakati alipozitwaa funguo za mauti, kuzimu, na kaburi, na kuvunja kila muhuri wa Kirumi, kisha akafufuka tena! Mbona, hakika.

Si ajabu yule mshairi alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

⁹⁶ Sawa. Alikuwa ni Mungu. Imanueli, hivyo ndivyo Yeye alivyo. Huyu Ndiye aliye usiku wa leo, “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kama Yeye si yule yule usiku wa leo, hakuwa hivyo wakati huo. Hiyo ni kweli. Yuko usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo, daima atakuwa vivyo hivyo. Naam. Sasa, Huyu hapo, Mungu alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe, akiwaonyesha Petro, Yakobo, na Yohana yale aliyokuwa anahitaji kwa Israeli.

⁹⁷ Sasa, katika Agano la Kale...Tunaona katika vitabu vya Agano Jipya, pia katika Wagalatia, na kwa hiyo, jinsi Paulo, akilielezea, Yeye alikuwa akimweka Mwana, kama vile katika Agano la Kale.

⁹⁸ Sasa, wakati baba mmoja alipokuwa na ninii kuu... Ufalme...Mnaona ha—hapa ndani, pia, katika Biblia, inasema katika Mathayo mlango wa 24, naamini ndivyo ilivyo, ama, la, ni Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, nitauchukua huo, tafsiri nyingine ya Kiingereza, ilisema, “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi.” Hilo si linasikika la kigeni kwetu leo? “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi.” Ati majumba makubwa, katika nyumba ndogo? Majumba mengi katika nyumba? Sasa, mnaona, kwamba...Sasa, ninii...Nao watafsiri, walitafsiri hilo, kwa ajili ya mfalme...Mnaona, katika siku hizo ufalme uliitwa “nyumba,” naye baba alikuwa mfalme juu ya nyumba. “Katika Ufalme wa Baba Yangu mna makao mengi,” ndiyo njia sahihi, njia ya Kiebrania ya kufasiri.

⁹⁹ Sasa, Moffatt aliifanya kuwa mbaya zaidi kuliko hapo awali, “Katika nyumba ya Baba Yangu kuna vyumba vingi,” kana kwamba tunaenda kule juu kuninii...Hiyo inaonyesha vile mtu wa kimwili anavyoweza kufanya na Neno la Mungu. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁰ Nilisimama, hapa si muda mrefu uliopita, huko Athene, Ugiriki, na kuona ile picha iliyochorwa ya kile wanachoitia *Adamu Na Hawa*. Huyu Hawa alikuwa ndiye kitu cha kuchukiza sana nilichowahi kuona maishani mwangu, naye Adamu alionekana kama jitu la zamani za kale. Mbona, inaonyesha ya kwamba, kile dhana ya kimwili ya uumbaji wa Mungu ilicho. Inahitaji Roho wa Mungu kufunua mambo, nalo Neno la Mungu linafunuliwa tu na Roho Wake. Hiyo ni kweli. “Limefichwa macho ya wenye hekima na akili, na kufunuliwa watoto wachanga, watakaojifunza.”

¹⁰¹ Hapa, Mungu alikuwa amesimama pale. Sasa, alikuwa akifanya yale hasa aliyowaambia wafanye. Sasa, katika urithi mkuu wa baba ambapo alikuwa, alikuwa na watu wengi wa kuajiriwa wakimfanyia kazi. Sasa, hili ni fundisho dogo hapa, natumaini haliudhi, bali ninataka tu kutoa hoja, kufanya imani ianze vizuri, ili kwamba tutakapoanza tutakuwa na mwelekeo mwema.

¹⁰² Angalieni, sasa, wakati mtoto mwanamume alipozaliwa katika familia hii, ya baba huyu, alizaliwa mwana, lakini hata hivyo, hakuwa na urithi kama tu mwana. Sasa, hapo ndipo ninafikiria ya kwamba sisi watu wa Full Gospel tuliachilia kidogo juu ya fundisho letu. Mnaona, tunamchukua mtu, twasema, “Vema, sasa yeye amejazwa na Roho Mtakatifu, yeye hunena kwa lugha, jambo ndilo hilo.” La, ndio kwanza uanze tu, ndio kwanza uzaliwe katika familia, hivyo tu. Hiyo ndiyo sababu, leo hii, kwamba sisi . . . makanisa yetu hayaendelei jinsi yanavyopaswa kuwa.

¹⁰³ Nafikiri, baada ya uamsho huu mkuu ambao umeenea ulimwenguni, katika miaka hii michache iliyopita, nafikiri watakatifu wa Mungu wanapaswa kuwa katika nyanda za mbinguni kila mahali, huku nguvu za Mungu zikiingia hospitalini, na kila mahali pengine, na ishara kuu na maajabu, na miujiza ikitendeka, bali hawezi kuwafanya watu, kusimama kimya muda mrefu vya kutosha. Kama tukipanda mbegu za kimadhehebu, tunavuna mavuno ya kimadhehebu. Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo tumefanya.

¹⁰⁴ Ukiangalia neno hilo, hapo, katika Kiebrania, “mvua ya masika na ya vuli,” *mvua ya masika* inamaanisha “mvua ya kupanda,” ndipo basi, Roho anaposhuka, huwashukia wenye haki na wasio haki, kama tumepanda mbegu za kimadhehebu, tutavuna tu mavuno ya kimadhehebu. Hivyo ndivyo tumefanya. Wabaptisti walichukua “milioni moja zaidi katika mwaka wa '44,” na ni vigumu kujua kile walicho sasa, baada ya yule mwinjilisti mashuhuri Billy Graham, na wengi wao, kufagia. Waangalie Wapentekoste wetu, kupitia kwa Oral Roberts, na Tommy Osborn, na watu mashuhuri namna hiyo.

¹⁰⁵ Vema, tumefanya nini? Tumeongeza washiriki, tuna makanisa bora zaidi, washiriki wengi zaidi, tunachohitaji ni ubora, sio wingi. Hiyo ndiyo shida. Huko ndiko kutafutwa kwa Bibi-arusi siku hizi. Eliezeri alikuwa na wakati mgumu sana akitafuta—akitafuta ubora, na halafu kumfanya awe tayari kuondoka ndilo jambo lililofuata, baada ya yeye kuupata. Kwa hiyo hilo—hilo ndilo jambo la pili la kufanya, tunamtafuta huyo sasa, Roho Mtakatifu, Mtumishi wa Mungu, kama alivyokuwa Eliezeri, anatafuta sifa hiyo, ule uhalisi, kile kitu ambacho hakitalighairi Neno la Mungu, kitasimama pale, kiishi ama kife, na kusema yaliyo kweli, “Mungu alisema hivyo, hilo latosha.”

¹⁰⁶ Ndiyo kwanza nimalize kuhubiri ibada ya juma moja, hapa chini, huko Grass Valley juu ya Ibrahimu, juu ya Uzao wake, na kadhalika. Jinsi ambavyo huyo Uzao halisi wa Kifalme wa Ibrahimu anavyolishikilia hilo Neno, haidhuru linasikika la kipuuzi jinsi gani ama chochote kile, anadumu moja kwa moja Nalo kwa sababu yeye ni Uzao wa Ibrahimu, hiyo ni kweli.

¹⁰⁷ Sasa, angalieni katika Agano la Kale sasa, mvulana huyu, wakati alipozaliwa katika familia, sasa, jambo la kwanza alilofanya baba, baada ya kuwa mtu mzima vya kutosha kuanza kufundishwa... Sasa, yeye ni mwana anapozaliwa, bila shaka, ana jina la familia, analo, bali hana urithi bado. Inakubidi kujua huyo atakuwa mtu wa aina gani kabla hajapata urithi.

¹⁰⁸ Sasa, baba, ili kuhakikisha ya kwamba mwana huyo alikuwa na mafunzo sahihi, alitafuta mwalimu bora sana ambaye angeweza kumpata. Wala kamwe hakumchukua mmoja ambaye angeridhiana apate kibali, ama kitu kama hicho, aseme, “Vema, nitatoa taarifa juu ya mvulana huyo, anaendelea vizuri, kwa sababu huenda baba akaniinua kidogo.” Atamtafuta mtu ambaye atamwambia ukweli. Naye...

¹⁰⁹ Na sasa, kama mvulana huyo alifanya vizuri sana, jinsi ambavyo mwa—mwalimu alipenda kumwendea baba yake kwa imani nzuri aminifu, na kumkabili, na kusema, “Naam, bwana, mwanao anaendelea vizuri.” Lakini jinsi ingekuwa ni aibu kama angeanda pale na kumwambia mvulana wake ni haini; jinsi angechukua kufanya hivyo.

¹¹⁰ Nami nashangaa, siku hizi, kwamba wakati Mungu ameliita kanisa Lake la Kipentekoste, yapata miaka hamsini iliyopita, sijui kama... Na wakati alipoliita Kanisa hapo mwanzo, aliweka Mwalimu wa aina gani juu ya Kanisa? Alimtuma Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu. Na siku hizi, tumelibadilisha kwa maaskofu, na makadinali, na mapapa, na kadhalika, pamoja na mawazo ya kila namna ya kikanisa na mafundisho ya sharti, ambayo yameongezewa na kuondolewa kutoka kwenye Biblia hiyo, hata watu hawajui la kuamini. Kweli. Hawajui waelekee wapi.

¹¹¹ Watu maskini, kama kundi la kondoo lenye mchu-... lisilo na mchungaji, kundi la bata bukini wasio na kiongozi. Hiyo ni kweli. Hawajui waruke waende wapi; kila kitu, kimeenda kila njia. *Huyu* anasema, “Njia *hii*,” na *hii*, “Njia *hii*,” na, mbona, hawajui la kuamini.

¹¹² Lakini Mungu alituma kwa Kanisa Lake, Roho Mtakatifu, huyo ndiye Mwalimu, naye huyo Mwalimu atasema kweli mbele za Mungu. Amina. Yeye huwalisha na kuwafundisha watoto Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Mungu atayahukumu makanisa, nilisema muda mfupi uliopita, kwa Neno Lake, Biblia ilisema, nilihisi hilo likinjia, Biblia ilisema

hapa ndani, ninii. . . Mungu atalihukumu Kanisa Lake kwa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Naye Yesu ni Neno, kwa hiyo ni Neno lililodhihirishwa, kama Kristo angali anadumu Kristo, Yeye hulichukua hilo Neno na kulidhihirisha. Amina. Haya basi. Ni Neno likiishi miongoni mwetu, likifanyika hai.

¹¹³ Sasa, huyu mwalimu, vipi kama mvulana huyo alikuwa mbaya sana? Yeye hakushughulika na kazi ya babaye? Angefanya tu chochote? Jinsi mwalimu huyo angeona aibu kwenda mbele za baba yake na kusema, “Bwana, na—nachukia kukwambia, lakini mvulana wa—wako hafanyi vizuri sana.” Nawazia ange—ange—angeona haya, ageuze uso wake.

¹¹⁴ Unafikiri Roho Mtakatifu hufanya nini, siku hizi, anapokuja mbele za Mungu Baba yetu, pamoja na ripoti kutoka kanisani, kwamba tumegawanyika katika madhehebu mia tisa mbalimbali, wala hawatashirikiana mmoja na mwenzake, na kila mtu ana *hiki*, *kile*, na *kinginecho*? Hakuna mtu. . . Walitaka tu kupata washirika wengi zaidi, kuwaingiza wengine wa *hawa*, na *wale*? Ninawazia Yeye anageuza kichwa Chake.

¹¹⁵ Ningeweza kusema jambo linalowaka moto hapa, huenda likaudhi, bali mwajua, hii ni nyumba ya masahihisho. Mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nina furaha mlisema hivyo, hilo linamaanisha, “Na iwe hivyo.”

¹¹⁶ Mnafikiri Mungu angefanya nini leo, wakati Roho Mtakatifu anapokuja na kumwambia kwamba, katika makanisa yetu, kwamba tumekubali mafundisho ya sharti badala ya Neno Lake? Mnafikiri nini, tunakubali kanuni za imani badala ya Kristo? Mnafikiri Yeye anafanya nini wakati ninii yetu. . . anapokuja na kusema ya kwamba binti Zake wote wamekata nywele zao, wanavaa kaptura, wanavuta sigara? Hiyo ni ninii. . . Biblia ilisema watu kama hao hawawezi kuingia. Kutokuamini. . .

¹¹⁷ Mnasema, “Haileti tofauti yoyote.” Usimwache ibilisi akwambie hilo. Kama Mungu alisema hivyo. . . Paulo alisema, *hapa* ndani, katika Wagalatia 1:8, “Kama Malaika kutoka Mbinguni akihubiri Injili yoyote isipokuwa hii niliyowahubiri, na alaaniwe.” Kwa nini ilileta tofauti kubwa sana? Hata kile kitu kidogo cha mke wa Lutu hata kugeuka, kuangalia juu ya bega lake, naye akageuka kuwa nguzo ya chumvi.

¹¹⁸ Huna budi kulichukua Neno. Kuna ulegevu mahali fulani. Huna budi kurudi kwenye Injili, kumrudia Kristo, kurudi kwenye Neno lililo hai, si kulikwepa kwa ajili ya kitu fulani *hivi*, huna budi kuliadini.

¹¹⁹ Vipi kama akienda, aseme, “Hawaamini katika uponyaji tena, mapigo Yako yalikuwa ni bure kwao, maana wanasema, ‘Siku ya miujiza zimepita’”? Loo, hana budi kuona haya anaposema hivyo mbele za Baba. Naam.

¹²⁰ Mnaona, hawa—hawaliadini. Wanaliondokea, siku baada ya siku wanaanguka mbali zaidi na zaidi. Mnajua hilo. Haikubidi

kuwazia juu ya... Baadhi yenu ninyi wazee mmekuwa kwenye jambo hili muda mrefu kuliko mimi, angalieni nyuma miaka michache iliyopita, jinsi ilivyokuwa: mikutano ya maombi ya usiku kucha.

¹²¹ Mnafanya nini usiku wa leo? Mnaondoka Jumatano usiku, labda kwenye saa kumi na mbili ama saa moja, labda hata hamji kwenye mkutano wa maombi, mnataka kwenda kuona kitu fulani kichafu cha televisheni, cha mwanamke fulani aliyeolewa mara nne au tano na mwanamume fulani, au mwanamume aliyeoa mara nne au tano, kisha msemi mnampenda Mungu, huku mnakaa mbali na mikutano ya maombi. Hiyo ni kweli. Mnaangalia *Tunampenda Lucy*, ama Elvis Presley, ama baadhi ya hao jamaa waliozua haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa supu ya de-...

¹²² Elvis Presley alikuwa ni mvulana wa Kipentekoste, aliyewapeleka watu wengi kuzimu kuliko Yuda angeliwahi kupeleka. Hakika, maana kuwachukua hawa wasichana wadogo, nao wanasema, "Mbona, yeye ni wa kidini sana." Msiamini kitu kama hicho. Ati wa kidini? Shetani yuko hivyo pia, vivyo hivyo na Kaini. Msiamini hilo. Ni kazi tu za ibilisi kuwapeleka ninyi watoto huko nje kwenye sakafu hizo pamoja na bugibugi hizi zote, na upuuzi huo wote, *Kujinyonga-nyonga*, na kila namna ya upuuzi huko nje, maisha machafu, nusu uchi.

¹²³ Baadhi yenu wanawake wa Kipentekoste, ni aibu. Hiyo ni kweli. Ninyi wanaume mtakaowaacha wafanye hivyo, ninyi ni wabaya kuliko wao, kwa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Mwanamume anapaswa kuwa ndiye mtawala wa nyumba yake mwenyewe. Hiyo ni kweli. Lakini tuna nini siku hizi? Si ajabu hatuwezi kuwa na imani. Si ajabu hakuwezi kuwa na ibada za uponyaji Marekani, tumemwacha Mungu.

¹²⁴ Si muda mrefu uliopita, nilisimama kule Afrika Kusini, mkutanoni siku moja na kuona yapata wanawake elfu kumi wenyeji, hawakujua mkono wa kulia wala wa kushoto, uchi kama walivyokuja katika ulimwengu huu, nao wakampokea Kristo kama Mwokozi binafsi. Basi walipokuwa wamesimama pale, huku wameinua mikono yao juu na kumpokea, walipoishusha mikono yao, walikunja mikono yao wapate kuondoka, wakajifunika sehemu kubwa kadiri walivyoweza; Roho Mtakatifu, Mwenyewe, akiwafanya wajue walikuwa uchi.

¹²⁵ Unawezaje kusema ya kwamba mwenyeji huyo avaae blanketi, asiyejua lolote kumhusu Mungu, anampokea Roho Mtakatifu na kutambua wako uchi, huku hawa wanawake wa Kimarekani wakivua nguo kila mwaka, na kudai kuwa, wakiimba katika kwaya, na ni Wakristo, wanadhaniwa kuwa...? Kuna kasoro mahali fulani, wala haiko kwa Mungu wala Biblia Yake, nanyi mnajua hiyo ni kweli. Si ajabu hatuwezi kuwa na miamsho, si ajabu hatuwezi kuingia katika jambo

hili kwa nguvu, si ajabu mambo hayawezi kutukia. Mwalimu anakuja mbele za Baba akitikisa kichwa Chake.

¹²⁶ Loo, jamani, wanavyofanya ni vibaya sana. Vema, hiyo ni kweli. Kuna shida gani? Maskini tikiti, tikiti ya posho ama chochote kile, ama—ama kitu fulani kidogo ambacho mtu fulani anaogopa kusema jambo fulani. Hilo ni Neno la Mungu, lihubiri ama uliache.

¹²⁷ Sasa, jambo la ajabu, mama fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, ni—nilitoa tamshi, baada ya kurudi, alikuwa . . . alikuwa amejipodaa rangi ya makucha kwa wingi, mnajua ninii—mnajua ninii . . . mnaitaje? Ninii . . . Nilimwona mmoja hivi majuzi. Kusema kweli, ni—nilijisikia ninii sana . . . Nilikuwa huko kwa Clifton kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, nami nilikuwa nimesimama kule chini, nikimngojea Ndugu Arganbright, aje, ndipo mmoja wa wanawake hawa akaja, ana mtindo mkubwa wa kukata nywele kichwa-maji, mwajua, moja ya hivyo vitu vikubwa namna *hiyo*. Sijawahi kuona mavazi kama hayo maishani mwangu, huyo—huyo huenda alikuwa ni mwanamke mwenye sura nzuri, lakini alionekana kama mnyama wa zamani za kale. Naye alikuwa amesimama pale. Si—sisemi hivyo kwa mzaha, hiyo ni . . . hapa si mahali pa mzaha, Hii ni Biblia, Hii ni Kweli ya Mungu.

¹²⁸ Naye huyo hapo alisimama akiwa na—akiwa na samawati juu ya macho yake na—na nyekundu juu ya hiyo, na, loo, ni—nikasema, “Mimi ni . . .” Ni—nimeona pelagra, nimeona ukoma, bali sijawahi kuona kitu kama hicho, nilifikiri mwanamke huyo—nilifikiri mwanamke huyo alikuwa mgonjwa, ndipo nikamwendea, nilikuwa nikitaka kumwuliza, uh, kumwambia, niseme, “Dada, samahani, lakini mimi ni mmishenari, ninawaombea wagonjwa. Naweza kukusaidia?” Na yapata wakati huo, hawa hapa wanakuja wanawake wawili au watatu zaidi vivyo hivyo.

¹²⁹ Nami nikawazia, “Humaanishi kuniambia hawa Wamarekani wanafanya hivyo!” Ningeweza kuwaona wenyeji *huko* nje wakifanya hivyo. Hiyo ni tabia ya kikafiri, ninaweza kuwaona wakiweka matope kwenye uso wao, na kadhalika, na kujipaka rangi, lakini hakuna kitu katika ninii, jinsi watu waliostaarabika wanavyopaswa kuwa. Nena kuhusu ustaarabu, sisi ni . . . ule mnara wa kale ulipembea nyuma. Hiyo ni kweli kabisa. Loo, aibu sana!

Nilisema jambo fulani kulihusu wakati mmoja, huyo mama akakutana nami nje, akasema, “Bw. Branham, nakupa ufahamu, mimi ni Mpentekoste.”

Nikasema, “Vema, Bwana asifiwe, basi tenda kama mpentekoste.”

Akasema—akasema, “Vema,” akasema, “unafikiri ni kosa, basi, kwa mwanamke . . . Ulinena kuhusu mwanamke kuvaa vazi la mwanamume?”

Nikasema, “Biblia ilisema . . .”

Akasema, “Mimi sivai kaptura,” akasema, “ninavaa suruali ndefu.”

Nikasema, “Hiyo ni mbaya zaidi; Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi, limpasalo mwanamume.” Kweli.

¹³⁰ Mungu hana kikomo, Mungu kamwe hawezi kubadilika, uamuzi Wake ni mkamilifu. Nionyeshe wakati mmoja ambapo Mungu hubadilika; Yeye habadiliki. Alitoa pendekezo, katika bustani ya Edeni, ya kwamba mahali pekee pa kumwabudu Mungu palikuwa ni chini ya damu, Naye kamwe hajapabadilisha, sikuzote pako, Yeye hupatukuza tu: “Mmewasikia wakisema, hao wa kale, ‘Usiue.’ Lakini Mimi nawaambia, ‘Kila anayemkasirikia ndugu yake. . .’ Mliwasikia wakisema, ‘Usizini.’ Lakini mimi nawaambia, ‘Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani. . .’”

Basi sikilizeni hapa, akasema, “Vema, nakuambia sasa,” akasema, “hawatengenezi nguo kama—kama hizo.”

Nikasema, “Wangali wanatengeneza cherehani na kuuza vitambaa, hakuna—hakuna udhuru, mnaona, uta—utaachwa tu bila udhuru.”

¹³¹ Sikilizeni, hebu niulize . . . niseme tu jambo hili moja, nitaliacha hili somo, maana hilo ni kwa ajili ya wachungaji wenu, bali ni—ninanii tu, kuwafanya mjue ninachowazia juu yake. Sasa angalieni, mtakapokuja kwenye Kizimba cha Hukumu, hivi ulijua unaweza kuhukumiwa, papo hapo, kwa kufanya uzinzi, na hata hivyo wewe u safi tu kama yungiyungi? Yesu alisema, “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani. . .” Na baadhi yenu wanawake mnawaachilia wasichana wenu waende huko nje, na—na kuvaa hizo nguo, na kutembea huko nje. Sasa, vipi kama mwenye dhambi huyo akishuka barabarani na kumwangelia mwanamke huyo kwa kumtamani? Yeye atawajibika kwa jambo hilo kwenye Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi. Ni nani aliyefanya jambo hilo? Ni nani aliyeye na hatia? Huyo msichana alikuwa, kwa kujiwasilisha namna hiyo. Hiyo ni kweli kabisa. Msifanye uadui na mimi, zungumzeni na Mungu juu yake. Hiyo ni kweli.

¹³² Lakini hilo ndilo . . . Roho Mtakatifu anakuja mbele za Baba, na kusema, “Tungewezaje kamwe kujenga Kanisa juu ya kitu kama hicho? Inawezekanaje . . . ?” Sikilizeni, enyi marafiki, wakati umewadia wa kusafisha . . . kutoka juu ya mimbara hata kwa bawabu kule chini, na kuanza upya.

¹³³ Ni kama tu kundi la . . . Hebu wachukue ndege, watage mayai yao katika majira ya kuchipua. Naye maskini mama ndege

anaweza kutaga kiota cha mayai, wala si lazima awe pamoja na mwenziwe, bali anaweza kutaga hayo mayai, na anaweza kubaki juu yao, anaweza kuyageuza, naye anaweza kukaa hapo mpaka ashikwe na njaa sana, mpaka awe mnyonge sana asiweze kutoka kwenye hicho kiota, nayo kamwe hayataanguliwa. Kwa nini? Yameoza; yanaozea moja kwa moja katika kiota.

¹³⁴ Na hiyo ndiyo shida leo hii, tuliwachukua tu washiriki *wengi sana*, na kadhalika, na kuwabembebeza *huku*, na kuwabembebeza *kule*, tuna kiota tu kilichojaa mayai yaliyooza. Wakati umewadia wa kusafisha kitu hicho kabisa, na kuwakutanisha hao watu na Mwenzi, Kristo Yesu, pamoja na Neno la Mungu, warudi katika matendo na nguvu, ndipo tutakuwa na uamsho ambao utatikisa kitu fulani na kufanya jambo fulani, ndipo mtamwona Kristo akijitokeza jukwaani juu ya zile nguvu, hawezi kuja maadamu mambo haya yanamzuia. Hiyo ni kweli.

Si ajabu Mwalimu anakuja mbele za Baba, anaona haya, na kusema, “Naam, kanisa Lako. . . Naam, najua linasema hivyo, bali wao—wao hawafanyi hivyo.”

“Unamaanisha hawafanyi?”

“Hawafanyi hivyo.”

¹³⁵ Haya basi. Ni fedheha jinsi gani! Ni sikitiko jinsi gani hilo halina budi kuwa mbele za Baba, wakati Mwalimu anapokuja, Roho Mtakatifu, na kuleta hiyo, maana Yeye ndiye Mwalimu wetu, tunajua hilo. Sasa, sasa, hili, ninii. . . Naye Roho Mtakatifu aliiandika Biblia, Biblia ilisema hivyo, “Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Biblia.” Kwa hiyo Biblia imeandikwa kwa uvuvio, hakuna tafsiri ya kibinafsi, ni jinsi tu ilivyoandikwa, papo *Hapo*. Ichukue tu, na uiamini, iweke katika matendo, Mungu ataitimiza. Sijawahi kumwona akiahidi chochote bado ila kile alichofanya; daima atafanya hivyo.

¹³⁶ Sasa, huyu hapa anakuja—huyu hapa Mwalimu anakuja. Sasa, vipi kama ninii Yake. . . Yeye anakuja mbele za Baba, jinsi anavyojisikia! Jamani! Anakuja, na kusema, “Loo, Mwanao anaendelea mbele! Yeye ni kama tu ‘mwana anayemshabihi sana babaye,’” kama tunavyosema huko chini kusini. “Yeye ni kama Wewe kabisa, yeye, anawajali sana wagonjwa wote na wanaoteseka, anavutiwa sana na wokovu wa watu, anavutiwa sana na haya yote, anaamini kila Neno ulilosema. Unajua nini? Yeye analiendesha kanisa jinsi tu Wewe ungeliendesha kama ungalikuwapo. Unajua jinsi Mwanao alivyoliendesha, alipokuwa huko?”

“Naam.”

“Hivyo ndivyo anavyofanya. Nawe unajua, ulikuwa umeandika Mle ndani, ‘Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.’”

“Naam.”

“Vema, hivyo ndivyo hasa wanavyofanya.”

Loo, jamani! Sasa, jinsi ambavyo Baba hana budi kusema, “Huyo ni Mwanangu! Huyo ni mtoto Wangu!”

¹³⁷ Hiyo ndiyo sababu angeweza kutabasamu *hapa*, Yesu alikuwa ametekeleza kila Neno lake. Jambo ndilo hilo. Alikuwa ametekeleza, sawasawa kabisa na Neno, sasa, kwa sababu Yeye alikuwa ndiye yule Mwana mkamilifu. Naye ni yeye yule, Naye alikufa apate kuwa Mzabibu, tupate kuwa tawi, ili aweze kututia nguvu kwa Uhai Wake tupate kufanya Uhai ule ule aliokuwa nao, uishi ndani yetu, ndipo tutafanya jambo lile lile.

¹³⁸ Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Sasa, tunaangalia yale aliyofanya. Mnaona, hatuna wakati, usiku wa leo, bali tutalichukua baadaye, na tuone kazi Zake zilikuwa nini, labda kesho usiku, halafu, tuone kama atafanya kazi zile zile, kama akifanya hivyo, Yeye hudumu yeye yule. Sasa, basi Mungu atapendezwa na jambo hilo.

Lakini tunapozunguka tukisema, “Vema, nawaambia, sisi ni wafuasi wa *Hili-na-hili*,” na . . .

Ni—nilimwuliza mwanamke mmoja wakati mmoja, kwenye mstari wa maombi, nikasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

¹³⁹ Akasema, “Nataka ufahamu,” akasema, “mimi huwasha mshumaa kila usiku,” kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote na Ukristo, kuwasha mshumaa kila usiku.

¹⁴⁰ Nikasema, “Vema, hiyo, si zaidi ya kulisha nguruwe kila usiku.” Mnaona? Nikasema, “Hilo lisingekuwa jambo la maana zaidi kwangu.” Nikasema, “Umezaliwa mara ya pili? Je, unamjua Kristo kama Mwokozi wako? Je, Yeye amekuwa uhalisi halisi ndani yako? Je, unaishi ndani ya Kristo? Je, Kristo anaishi ndani yako?”

¹⁴¹ “Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, ninyi. . . nami ndani yenu.” Jambo ndilo hilo. Mungu akiishi miongoni mwa watu Wake, hiyo ndiyo njia.

¹⁴² Ndipo tunaona katika siku hii. . . Sasa, tunachukua. . . Kama mwana huyo alikuwa ni mwana mzuri, alikuwa hasa. . . Sasa, kumbukeni, alikuwa ni mwana aliyezaliwa, sasa msikose hili, yeye alikuwa ni mwana aliyezaliwa, lakini mwaka baada ya mwaka aliendelea mbele. Sikuzote alikuwa katika shughuli za Baba, alifanya kazi jinsi Baba alivyofanya hasa.

¹⁴³ Jinsi yule Mwalimu alivyosema, “Loo, hilo ni zuri sana!” Mwambie Baba, “Mbona, ni jinsi hasa Wewe ungeliendesha kama ungalikuwapo. Alikemea *hili*, akahukumu *hili*, akalipa *hili* nafasi, amefanya jambo *hili* jinsi hasa ufanyavyo Wewe, hakuna tofauti, vivyo hivyo hasa. Ni kama tu Wewe, hapo. Ni maisha Yako ndani Yake hakika, maana. . . Hakika unaweza kujua yeye ni mwana wa Mungu, maana alizaliwa anayefanana na Wewe.” Mnaona? “Yeye hufanya jambo lile lile, hudumu moja kwa moja

na Neno Lako, kamwe hakosi Neno, hukaa moja kwa moja ndani Yake, hulisukuma moja kwa moja.”

“Loo,” Baba hana budi kusema, “hilo ni zuri sana.”

¹⁴⁴ Ndipo ikaja siku basi, kama mwana huyu aliendelea, ikaja siku, kile wanachoiita, “Kuwekwa mwana mahali pake.” Ndipo baba akakusanya kundi la watu, mjini, akamchukua mwanawe mwenyewe, na kumvika vazi la kupendeza, na kumweka juu sana hivi kwamba kila mtu angeweza kuona, akafanya sherehe, naye akampa mamlaka mwanawe mwenyewe aliyezaliwa nyumbani mwake, ama “akamweka mahali” pake. Basi alipofanya hivyo, jina la huyo mwana, baada ya hapo, lilikuwa sawa tu na jina la baba, kwenye hundi, ama chochote kile. Sahihi yake, siku hizo, ilikuwa ni muhuri, pete, maana wengi wao hawangeweza kuandika. Lilikuwa ni kosa la kufungwa gerezeni kuwahi...kunakili muhuri huo. Nao iliwabidi kufanya hivyo, nyuma ya ile pete nao wangeifinyilia, namna *hiyo*. Naye angeweza kuvaa pete ya baba yake. Kwa nini? Jina lake lilikuwa sawa tu na la baba.

¹⁴⁵ Sasa, hilo ndilo Mungu analojariibu kulifikisha Kanisa Lake, kufikia mahali ambapo sisi ni wana na binti za Mungu. Mnaona? Lakini ni...Sisi ni—sisi tunahangaika. Tunaachilia kila kitu...Na sasa, u—ulimwengu, ukijariibu kuzima kabisa kitu kilicho halisi, unajariibu kuwafanya watu waogope ukomunisti. Usiogope ukomunisti, huo si kitu.

¹⁴⁶ Ukomunisti...Ninataka kuwaulizeni ninyi wanafunzi wa Biblia jambo fulani. Ninataka mtu fulani anitolee Maandiko, mahali popote, kwamba ukomunisti utawahi kuutawala ulimwengu. Mbona, ukomunisti ni kitu tu kinachotumika mikononi mwa Mungu, kama ukisoma Biblia, kumteketeza yule kahaba, kumtesa. Ukomunisti hautautawala ulimwengu, bali Biblia ilisema ya kwamba Urumi utautawala ulimwengu. Nanyi mnaliona, sasa hivi, katika White House na unaanza. Kwa hiyo, ninyi maskini Wanademokrasia, mnaona, endeleeni (Vema, vema.), huku mnauza haki zenu za mzaliwa wa kwanza kwa supu ya siasa. Nitanyamazia hilo. Lakini ngojeni...

¹⁴⁷ Hata hivyo, hebu tulirudie hili, turudie kuwekwa mwana mahali pake. Wakati baba alipomweka mwana huyo mahali pake, basi chochote alichofanya, kilikubalika na baba yake, kwa kuwa alikuwa na muhuri wake.

¹⁴⁸ Sasa, hapo ndipo Kanisa linapaswa kuwa leo. Baada ya kumwona Mungu, kuona nguvu Zake, inapaswa kuwa kwamba Kanisa litoke moja kwa moja na kusema, “Katika Jina la Bwana Yesu Kristo,” kutumia Jina la Baba, kuliona likitimia, “BWANA ASEMA HIVI!”

¹⁴⁹ Sasa, Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe,” Yohana Mtakatifu 5:19. Tunapaswa kuwa katika hali ambayo hata Baba angetuonyesha

chochote, basi liangalie, kamilifu kabisa, linatukia kila wakati, namna *hiyo* tu. Mnaona? Ni kama tu... Hilo hapo. Hapo ndipo mwana amewekwa mahali pake. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa, kuwekwa mahali petu katika Kristo. Loo, ingekuwa ni wakati wa jinsi gani.

¹⁵⁰ Jinsi kanisa limepungukiwa! Jinsi ambavyo tumechukua miamsho mikuu na kuitumia kwa faida yetu, badala ya kiroho, kuwaingiza watu ndani kama wana na binti halisi wa Mungu, waliojazwa na Roho tukiwaka moto mioyoni mwetu mchana na usiku.

¹⁵¹ Kumbukeni, Biblia ilisema, “Roho Mtakatifu aliwatia muhuri wale tu waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa mjini.” Ninapenda kumchukua mchungaji wenu, niwachukue wale wachungaji wengine kule, “Je, una... Ni washiriki wangapi wa kanisa lako, wanaolala kifudufudi, na kulia kila usiku, kila siku, kwa ajili ya machukizo yanayofanyika mjini?” Hapo. Mnaona, ile bidii yote imekwisha kabisa.

¹⁵² Tumeangalia huko nje, mpaka tukapata kanisa zuri, tunalo jengo zuri sana. Hilo ni sawa, sina la kusema dhidi ya hilo. Madhehebu mazuri, hakuna hata neno moja dhidi ya hilo, hilo ni sawa, Sina neno dhidi ya hilo. Lakini kile ninachojaribu kusema, mnaliacha Jambo lililo muhimu. Mnaacha Jambo lililo muhimu: Kristo wa kanisa hili, Kristo katika madhehebu haya, Kristo ambaye... Mnayaangalia madhehebu, mkiangalia kanisa badala ya Kristo, naye Kristo ni Neno, nalo Neno ni hakika.

¹⁵³ Sasa, hilo ndilo tunalotaka, enyi marafiki. Hilo ndilo tunalotaka kuona juma hili, sivyo? Tunataka kumwona huyo Kristo, akitembea moja kwa moja hapa chini, sio kuja kwako na kusema, “Loo, mchungaji mpendwa, ndugu wapendwa, ndugu zangu wachungaji, ninawajulisha, dhehebu lingine ambayo litashinda Assemblies of God, ama Church of God, ama ninii... yote *haya*, *yale*, ama *mengineyo*. Vema, siku moja tutawashinda Wakatoliki.” Sasa, upuuzi huo. Ambapo, huenda ikawa ni sawa, lakini tumechelewa sana kwa upuuzi kama huo. Tunawezaje kuhubiri kuja kwa Kristo kumekaribia na kutenda jinsi kanisa linavyotenda siku hizi? Mamilioni ya dola katika majengo, na kadhalika, na kutenda... na kusema Kristo yuaja, mbona, matendo yetu wenyewe yanahukumu yale tunayozungumzia. Sasa, hiyo ni kweli.

¹⁵⁴ Simaanishi kuwa mkali, enyi marafiki, lakini hebu tuliweke hapa chini. Hebu na tuliangalie. Hiyo ndiyo sababu. Hatuna budi kurudi kwenye Neno hili. Hatuna budi kumrudia Mungu wa Neno, nalo Neno ni Mungu. Mnaona?

¹⁵⁵ Sasa, Yesu alikuwa amepitia jaribio na majaribu, na, “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na kujaribiwa. Kama hawezi kustahimili kurudiwa, anakuwa mtoto haramu, wala si mtoto wa Mungu, mwana wa Mungu.” Hiyo ni kweli.

¹⁵⁶ Sasa, angalieni waliolala hapa, katika—katika ninii yetu . . . Angalieni, wagonjwa na wanaoteseka waliolala hapa. (Sisemi hao ni wachungaji wanaofanya hivyo, sasa, hiyo huenda ikawa ni watu.) Nao wanasema, “Vema, labda, wametenda dhambi?” Si—sijui, hiyo ni juu ya Mungu.

Lakini wakati mmoja kulikuwa na mtu . . . Yeye alisema, “Ni nani aliyetenda dhambi, yeye, ama baba yake, mama?”

Kasema, “Hakuna, bali ili kazi za Mungu zidhihirishwe.”

¹⁵⁷ Je, lingekuwa jambo zuri kuona kila moja ya vitanda hivi na viti vya magurudumu vikifanywa tupu, hapa katika siku mbili ama tatu usiku? Hilo si lingekuwa ni jambo tukufu? Ndipo dhihirisho la Mungu litakuwa hapa. Si lingekuwa ni jambo zuri sana kumwona Roho wa Mungu akiingia miongoni hapa na kuanzisha uamsho miongoni, mpaka ingekuwa sikuzote ni mtu kulia mchana kutwa na usiku kucha, nao mkutano hata haungefungwa, unaendelea tu usiku kucha na mchana kutwa? Watu hata wasingetaka . . . hata kuona njaa, wakae tu hapa, wakila tu wema wa Mungu.

¹⁵⁸ Magazeti yangukuwa yakandika kila mahali, namna *hiyo*, huku watu wakitoka kwenye Maonyesho ya Ulimwengu kuona ni onyesho la aina gani Mungu alikuwa akionyesha, hiyo ni kweli, wakitoka Seattle kwenda Spokane. Inaweza kutokea. Acha Mungu aingie miongoni mwetu.

¹⁵⁹ Sasa, tunamwona Mungu, sina budi kufunga sasa katika hili, Mungu akisimama pale, basi angalieni, Yeye alimpandisha juu Mwanawe Mwenyewe, baada ya ninii Yake . . . Kumbukeni, Yeye alienda moja kwa moja mpaka Kalvari kutoka huko. Na akampandisha Mwanawe Mwenyewe kule juu. Naye alifanya nini? Alimwonyesha katika Kuja Kwake, alikuwa akimtukuza. Huyu hapo amesimama pale, na “Mavazi Yake yakang’aa kama jua.” Kwa maneno mengine, Mungu alisema, “Nimekuwa Baba Yako kote katika wakati, lakini sasa, njia pekee ya kunikaribia Mimi, tangu sasa na kuendelea, ni kupitia Kwake. Huyu ni Mwanangu mpendwa.” Mnaona kile alichokuwa akifanya? Kule kufanywa wana wenye mamlaka, kuwekwa mahali pake. Mnaona? “Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye.”

¹⁶⁰ Sasa, Petro, alisisimkwa alipoona mambo ya kimbinguni. Hiyo ndiyo shida siku hizi. Wanaona mambo ya kimbinguni, nao wote wanasimkwa. Hilo ndilo lililoanzisha jambo la kwanza kabisa, wakati baraka za Kipentekoste zilipoanza kuwashukia Wapentekoste miaka mingi iliyopita; nadhani hata sikuwa nimezaliwa wakati huo, lakini nimesoma vitabu vyao. Ndipo Roho Mtakatifu akawashukia, kisha Mungu akaanza kulirudishia Kanisa karama za kunena kwa lugha. Ndipo wote wakasisimkwa, na mmoja akasema, “Anakuja amepanda farasi mweupe; yuaja juu ya wingu jeupe. Vema, tutajiundia tu dhehebu letu wenyewe.”

Ndipo wakawashusha watu, nao wakaninii... wakaingiza kila kitu kanisani, na kuninii tu... badala ya kuachana tu nacho.

¹⁶¹ Israeli hawakujua hata kidogo, walipokuwa wamemwona Mungu akiya kule juu, walidhani ule Utawala wa Miaka Elfu ulikuwa umewafikia, walikuwa wamemwona Mungu akiwapiga hao Wamisri, na kuwazamisha katika Bahari ya Shamu, na kufanya ishara za kila namna, huku wamesimama pale ukingoni, naye Miriamu, akiwa na hiyo tari, akipiga na kupaza sauti, na kuruka-ruka, naye Musa akiimba katika Roho, mbona, hawakuwa ila yapata siku tatu mbali na ile nchi tukufu, hawakujua walikuwa na miaka arobaini mbele yao bado. Wala Wapentekoste hawakujua wakati Roho Mtakatifu alipowashukia kwa mara ya kwanza.

¹⁶² Lakini mnaona, mahali walipofanyia kosa lao la kijinga palikuwa ni Kutoka 19, walipoondoka kwenye neema ambayo Mungu alikuwa tayari amewapa, kisha akawapa nabii, na Nguzo ya Moto, na dhabihu, na kufanya ishara na maajabu. Neema ilikuwa imewapa hayo, lakini walitaka kitu cha kufanya wao wenyewe, iliwabidi kuwa na kitu cha kujifanya wenyewe madaktari wa uungu, kwa hiyo walitaka torati. Hapo ndipo walipokufia, nao wakakaa papo hapo mpaka wale wapiganaji wote wa kale wakafa. Hiyo ni kweli. Ndipo Mungu akaja, na kuchukua kundi jipya, na kuvuka Yordani pamoja nao.

¹⁶³ Pentekoste imekaa nyikani siku hizi, jambo lile lile, ikizungukazunguka, ikizunguka kilima kile kile. Mliwahi kuwazia walilofanya? Wakawaoza vijana, wakawazika wazee, wakawabusu watoto wachanga, na wakakuza mazao, na kufanikiwa. Na hilo ni sawa, lakini, ndugu, kuna Nchi ya Ahadi huko ng'ambo, ambapo mambo yote yanawezekana kwake aaminiye. Kila ahadi katika Kitabu hiki ni mali ya Kanisa. Kristo ni Neno la kuingia moyoni mwa mtu na kulidhihirisha Neno hilo. Mnaona?

¹⁶⁴ Tuliridhika tu, "Vema, nilinena kwa lugha." Hilo ni—hilo ni zuri. "Unaona, Ndugu Branham, nimempata," na kutenda jinsi unavyotenda? Ninalitilia shaka. "Kwa matunda yao mtawatambua." Maji huanguka juu ya ngano na juu ya magugu pia, mwajua, "Kwa tunda lao wanajulikana." Sasa, tunaona jambo hilo.

¹⁶⁵ Sasa, huo ndio tunaohitaji, ni uamsho. Tunahitaji ninii—ninii, si ninii, ninii tu—ninii—ninii [Kengele ya saa ya Ndugu Brsanham inalia—Mh.] kusanyiko la kikanisa, bali uamsho.

¹⁶⁶ Msisisimkwe, hiyo ilikuwa ni kengele ya saa yangu, nami... ikiniambia ya kwamba mimi... Kanisani kwa mara ya kwanza, kwa kawaida, sihubiri kwa muda mrefu sana, takriban saa sita, lakini wakati huu nilikuwa na kengele kule juu, na nilikuwa na saa mbele yangu, kwa hiyo ni sawa. Nina saa ndogo ya kengele ambayo kwa kawaida huniambia ni wakati wa kufunga. Kwa

hiyo basi, kuna mengi sana ya kusema, mengi sana ya kufanywa. Nina kundi zuri la watu hapa.

¹⁶⁷ Kwa nini hatuwezi kuwa nao? Kwa nini Kristo hawezi kuwa yeye yule kwetu? Kwa nini hawezi kuwaponya wagonjwa? Ndio kwanza afanye hivyo, hapa hivi majuzi usiku, huko Grass Valley. Niliona kila kiti cha magurudumu, kila kitu kilichokuwa mle ndani, kimefagiliwa kabisa, hakuna mtu mnyonge miongoni mwetu; wakatoka moja kwa moja pale, pasipo na hata mtu mmoja mnyonge. Hiyo ni kweli. Waliketi kimya, na kusikiliza mpaka wakalishika, na ndipo walipolishika, hilo hapo likaenda, nao...hakukuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu, karibu mara nne au tano ya kundi hili na, naam, mara nyingi; tulikuwa kwenye jumba kubwa la mikutano. Kwa hiyo basi, sasa angalieni, inaweza kufanyika, lakini mnaona, inawabidi kuwa na subira, inawabidi kuwa tayari, na hamna budi kuwa na Kristo.

¹⁶⁸ Sasa, ngojeni, kufikia kwenye mwisho tu sasa. Petro alisisimkwa sana na kusema, “Hebu...” Mwajua, mambo ya kimbinguni kwa kawaida huwafanya watu wasisimkwe. Mwajua, Israeli walisimkwa kule chini, badala ya kuingia chini ya ule upatanisho, kulikuwa na kundi la wasiotahiriwa lililoambatana nao, “kundi la watu waliochanganyika,” Biblia inawaita. Lilisababisha shida baadaye kidogo. Mambo ya kimbinguni yalikuwa yamefanywa, na kulikuwa na umati mchanganyiko ulioambatana nao.

¹⁶⁹ Ni jambo lile lile lililotukia kwa uamsho huu, waaminio nusu nusu. Kuna matabaka matatu tu ya watu ulimwenguni, hayo ni: waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, nao wameketi katika kila kundi. Kwa hiyo unalipata. Naam. Jambo ndilo hilo. Kwa hiyo basi, tunaangalia.

¹⁷⁰ Huyu hapa. Sasa, Petro alitaka, upesi sana, alitaka kuwa na hati miliki ya kitu hiki, kasema, “Hebu na tuanzishe madhehebu matatu kutoka kwake. Tutajenga kibanda hapa Chako, pia tutajenga kimoja cha Musa, kisha tujenge kimoja cha Eliya. Tutakuwa na...Tutaanza tu moja kwa moja hapa, tukiwa na vitatu kwa kuanzia.”

¹⁷¹ Sasa, loo, ni jambo la jinsi gani. Nina furaha ya kwamba yeye...halikufanikiwa, maana ni—nisingetaka kuja kwa Musa. Musa aliwakilisha torati, na torati haina nguvu za kuokoa. Torati inaweza tu kukutia gerezani, haiwezi kukutoa. Torati haina neema kwake. La, bwana. Torati ilikuwa mwalimu, nayo torati ilituhukumu tu. Torati ilituonyesha tulikuwa wenye dhambi, lakini haikuwa na neema kwake.

¹⁷² Basi, ni nini...Eliya aliwakilisha nini? Haki, manabii. Rehema, hatutaki haki Yake. Kama ningeipata haki, ninge kuwa nimekufa, na sisi sote tungekufa. Hatutaki haki. Nisingetaka

haki, mimi...ningehukumiwa. Hatutaki haki Yake, sitaki haki ya Mungu.

¹⁷³ Lakini, “Alipokuwa katika kunena...” Kasema, “‘Na tujenge vibanda vitatu hapa.’ Naye alipokuwa katika kunena...” Nina furaha sana Mungu alimkatiza. Naam. Yeye alisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye.” Yeye hajali unaanzisha madhehebu mangapi, na unaanzisha *haya* mangapi, na unaanzisha kiasi gani cha *haya*. “Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye.” Ana nini kwa ajili yangu? Yeye ana neema, ana msamaha, ana uponyaji, ana wokovu.

¹⁷⁴ Kwa hiyo, usiku wa leo, siji kama dhehebu, ninakuja, nikiketi pamoja na ndugu zangu, kila mmoja wao, ninawapenda kila mmoja, madhehebu yote, bali ninakuja kuwakilisha Mtu mmoja kwenu, Mwana mpendwa wa Mungu, Yesu Kristo, “Msikieni Yeye.” Na tuinamishe kichwa chetu, kwa muda kidogo tu sasa.

¹⁷⁵ Unaamini, usiku wa leo, kwa moyo wako wote? Si kuliwazia tu, si kulikubali kwa kanuni ya imani, bali kulikubali kwa sababu wewe, ndani ya moyo wako na nafsi, unajua hilo, ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, unaliamini. Mungu awabariki. Sijui ni wangapi hapa, na huko juu kwenye roshani sasa, ambao si Mkristo, nao wangetaka kuja kumsikiliza Kristo? “Msikieni Yeye.” Hayo maneno matatu madogo, “Msikieni Yeye,” kama utamsikia, maisha yako yatabadilishwa, usiku wa leo. Nanyi mliorudi nyuma, mliomjua wakati mmoja kisha mkamwacha, “Msikieni Yeye.”

¹⁷⁶ Nanyi msio na Roho Mtakatifu, na mnajua ya kwamba *hiyo*, hamna budi kuwa na *hiyo* Mbegu iliyorutubishwa la sivyo haitachipuka...Ninyi wakulima mnajua hilo. Kama mbegu hiyo haijarutubishwa, haidhuru inaonekana nzuri jinsi gani, haitaishi. Haidhuru unaweza kuiga maisha ya Mkristo kiasi gani kwa kuishi vizuri, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kuwa na huyo Roho Mtakatifu; huna Huyo, basi njoo “Msikie Yeye.”

¹⁷⁷ Nanyi wagonjwa humu ndani, wengine wakiwa na ugonjwa wa moyo, wengine kwenye viti vya magurudumu, wengine watakufa mara moja Mungu asipokufanyia jambo fulani, hivi hutamsikia? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Usife moyo sasa. Nataka umsikie, umwamini, ninawatakeni mwamini ya kwamba Yeye yupo hapa na atawajalia.

¹⁷⁸ Sasa, ninyi huko nyuma, huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, na kila moyo ukiomba, wewe ambaye ni mwenye dhambi na humjui Kristo (Na kuanzisha mkutano vizuri, hebu na tumthibitishie Mungu ya kwamba tunampenda.), njoni hapa karibu na madhabahu na tuombe. Sivyo? Inuka kutoka kitini mwako, njoo. Rafiki mwenye dhambi, popote ulipo, njoo, msikie Mwana wa Mungu akinena amani moyoni mwako, amani kama mto. Utakuja?

...kutangatanga;
 Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
 Ee, Bwana, naja...

Sasa, hujawahi kuona mwujiza, unasema, "Sijawahi..." lakini kabla hujaona chochote, njoo, mkubali Kristo kwanza.

Naja...

Ndipo mtakapokuwa tayari kukubali miujiza, na kadhalika, mtakapowaona viwete wakitembea na vipofu wakiona.

Loo, kamwe...

¹⁷⁹ Hivi majuzi usiku, mama mmoja aliyekuwa na mtoto mchanga aliyekuwa na kichwa kilichojawa maji, huko juu kabisa...Mungu akubariki, Dada. Alikuwa na mtoto huyu mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji. Tulimwomba tu. Wakampeleka kwa daktari, kesho yake asubuhi, da-daktari akasema, "Imekuwa je kwa mtoto huyu?" Liliwashtua majirani, eneo lote huko, kichwa kikapungua, kawaida, kikarudi, ni sawa.

...naja nyumbani.

Njoo, uone muujiza ulio mkuu kuliko yote: Kristo, kuubadilisha moyo wa mwenye dhambi.

...nyumbani, naja nyumbani,
 Kamwe...

Hivi hutasimama uje? Vipi kukuhusu wewe sasa, ambaye umepotea mbali na Mungu? Na wewe je? Utakuja? Ninaweza tu kukuuliza, unajua. Ni uamuzi wako.

...Mikono Yako ya upendo,
 Ee, Bwana...

Je, umetangatanga mbali na Yeye? Njoo huku, usiku wa leo, pamoja na mwanamke huyu, *hapa*. Mungu awabariki. Njoo huku, tunakualika. Njoo huku sasa hivi. Hiyo ni kweli.

Naja...

Vipi huko juu kwenye roshani? Tutakungojea, watu wataondoka kwenye vipandio, nanyi mnaweza kushuka moja kwa moja. Shukeni moja kwa moja, tunaninii...tunawangojea.

Loo, kamwe sitatangatanga tena;
 Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
 Bwana, naja nyumbani.
 Naja...

Rafiki uliyerudi nyuma, laiti ungekuja; utaanzisha uamsho moja kwa moja kama utafanya hivyo. Fanya amani yako mwenyewe. Hiyo ni kweli.

...tangatanganga;
 Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
 Sasa, Bwana, naja...(...?...)

¹⁸⁰ Sasa, wakati nyimbo zingali zinapigwa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Ukitaka kuona uamsho ukianza, uanzishe ndani yako mwenyewe. Unaona? Hauna budi kuanza ndani yako. Imani haina budi kuanza.

¹⁸¹ Sasa, vipi kuhusu baadhi yenu ninyi watu ambao ni wafuasi wa kanisa? Niliuliza hili huko Grass Valley, hivi majuzi usiku, kabla ya kule *kusafisha*, tulikokuwa tukizungumzia, nami nikawauliza wanawake hao wote, waliokuwa wamekata nywele zao na kuvaa nguo na kadhalika, nikawauliza, hata wahudumu walisimama na kukiri kwamba walikuwa wamekosea, ndipo Roho Mtakatifu akaingia.

¹⁸² Huna budi kujiweka sawa, rafiki. Mungu hatajenga msingi juu ya kitu kitakachoanguka, halina budi kujengwa—kujengwa juu ya, si kusisimkwa kiakili, na mhemuko, halina budi kuja kwa Neno la Mungu. Uko tayari kukubali kwamba umekosea, ewe mfuasi wa kanisa? Utakuja hapa juu na kuomba pamoja nami? Nitaomba pamoja nawe.

¹⁸³ Njoni sasa, baadhi yenu watu mnaojua ya kwamba mmekosea, angalieni jinsi mlivyo waaminifu, utapanda hapa mbele za Mungu, useme, “Ninatambua nimekosea, nitalirekebisha.”

¹⁸⁴ Mungu akubariki, Mama. Hiyo ndiyo njia ya kupata kitu kutoka kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki, Bibi mdogo. Hiyo ni kweli. Tunapaimba tena, njoni sasa, mshiriki wa kanisa, wanaume, wanawake, yeyote yule, njoni mpige magoti hapa. Tunajua kama tumekosea, hebu tukubali kwamba tumekosea. Nini...? Usibahatishe, hutapata nafasi tena. Wewe... Vipi kama ukifa usiku wa leo?

¹⁸⁵ Huko Los Angeles nilikuwa nikihubiri juu ya wokovu, kule kwenye Ikulu ya Ng’ombe, kwenye Lango la Kusini, nami nilikuwa nikihubiri juu ya wokovu, mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, alikuwa ameahirisha wokovu maishani mwake mwote, akaja madhabahuni, na kujazwa na Mungu usiku huo, akaenda nyumbani, kisha akaenda kwa Mungu, akaenda nyumbani na kukutana na Mungu. Neema ya Mungu, wazia jambo hilo, miaka hiyo yote kisha akaja wakati huo wa mwisho. Vipi kama angaliukosa wakati huo? Usiku wa leo, yeye yuko katika amani ya Mungu. Kama angaliukosa hiyo, angekuwa amekwisha milele.

Njoo sasa. Hivi hutakuja tunapaimba tena? (Dada, wewe, ninyi nyote.)

Naja nyumbani...

Njoo, Ndugu; njoo, Dada, hebu tuje karibu na... Hilo ni sawa. Baba fulani mzee akipiga magoti hapa chini, kuomba.

Kamwe... kutangatanga;

Fungua wazi mikono Yako ya...

¹⁸⁶ Mshiriki wa kanisa, unajua. Ni wangapi hapa ndani wamekuwa kwenye mikutano yangu hapo kabla (Inueni mikono yenu.), mikutano ambayo Bwana amenipa? Basi ninyi nyote mnajua ninalozungumzia, Roho Mtakatifu. Chini ya upambanuzi, ninaangalia dazani mbili au zaidi, papo hapo, wanaopaswa kuja. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ndiyo sababu ninashikilia jinsi ninavyoshikilia. Njoni.

¹⁸⁷ Hebu tukabiliane nayo sasa hivi, enyi marafiki. Huenda mkafikiri ninajaribu kuwakemea, siwakemei. Mungu anajua hilo; niko hapa kuwasaidia. Afadhali niwe nyumbani pamoja na familia yangu, mahali pengine, kuliko kuwa nimesimama hapa mdanganyifu, ama mnafiki, nife baada ya maisha haya yote ya kuhangaika kote ulimwenguni, na kila kitu, nikiiacha familia yangu na kadhalika, na wapendwa wangu, na kusimama hapa.

¹⁸⁸ Mnajua siji kwa ajili ya pesa. Je, nimewahi kuwaomba pesa? La, bwana. Je, nimewahi kujaribu umaarufu? Ninaliepuka, sina televisheni, redio, chochote. Sina kitu. Nimekuja ili niweze kuja kwenye makanisa madogo na kadhalika, na kutoka hapa nje; ninakuja kwa sababu ninampenda. Ninaweka mabega yangu pamoja na hao ndugu, na kujaribu kusukuma kila kitu katika Ufalme wa Mungu.

¹⁸⁹ Mlisoma katika *Sauti* ya Wafanyabiashara ya maskini kile kitu kama kuhamishwa, nilikopata hivi majuzi, nikaona Mbingu na wapendwa hao wote, nami nikamwona mwanamke huyo, mwenye umri wa miaka tisini, alikuwa amemjia Kristo, kijana huyo mpendwa.

Kasema, “Hivi humkumbuki?”

Nikasema, “Simkumbuki.”

¹⁹⁰ Sasa, hamwezi kuthubutu kuikosa, enyi marafiki. Basi kumbukeni, kufasiriwa vibaya kidogo kwa Neno kulizua *haya* yote... kungelizua *haya* yote yasitendeke. Njoni. Hebu tuwe halisi—hebu na tuwe wanyofu sana nalo. Hebu—hebu tuje.

¹⁹¹ Na sasa, kama mtafanya hivyo, ulipoinua mkono wako, utaona, utaona ya kwamba Mungu atajibu. Mnaona, shida yake ni kwamba, inapita moja kwa moja na kusema, “Naam, ninaamini hiyo ni kweli.” Lakini unamaanisha unamwacha Shetani ashindilie hilo kwako na kulizima kabisa, wakati unajua mahali pako ni papa *hapa*? Ninaweza kuwaambia hiyo ni “BWANA ASEMA HIVI.”

¹⁹² Sasa, ninyi angalieni mikutano iliyosalia, angalieni jinsi inavyofanya kazi, mwone kama siwaambii ukweli. Usiku wa kwanza ambao nimewahi kufanya mkutano bila kuwa na mstari huo wa maombi, kwa kuwa ninafanya yale hasa Roho Mtakatifu aliyoniambia nifanye, “Weka msingi huo kwanza,” maana niliona, likitukia papo *hapo*, “kisha ujenge kutoka hapo.” Vema. Mshiriki wa kanisa, aibu kwako. Mara moja zaidi, enyi wasichana, mkipenda, ninyi nyote.

Naja...

¹⁹³ Bwana Mungu, tafadhali, naomba, Baba, haya ndiyo yote ninayojua kufanya. Mhukumu kila mtu aliyekosea, Bwana, wanajua wamekosea. Ninaomba ya kwamba utalijalia, Bwana, kwamba waweze kuuona utukufu wa Mungu hata wa leo bado, kwa maana Nuru za jioni zinakaribia kuangaza, jua linashuka.

¹⁹⁴ Ninaomba, Baba, kwa ajili ya neema na rehema, uturehemu, Bwana, ninaomba tunapokungojea Wewe. Tujalie, Bwana. Waokoe hawa wanaoweza kuokolewa sasa, ujipatie utukufu, usiache mkutano udidimie kwa sababu ya wengine. Ninaomba ya kwamba utatujalia, usiku wa leo, Bwana, katika Jina la Yesu.

Naja nyumbani, naja nyumbani,
Sitatangatanga tena;
Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
Sasa, Bwana, naja nyumbani.

¹⁹⁵ Sijui, ni wangepi, huko nje, ambao kweli wanajua kuomba, wanaomwamini Mungu, na unajua ya kwamba unaishi juu ya mambo yote ya ulimwengu kwa neema ya Mungu? Mambo ya ulimwengu hayawasumbui, mitindo na uchafu wa Hollywood ambao umechukuliwa...Kumbukeni, ustaarabu umesafiri pamoja na jua; hii ni Pwani ya Magharibi, hapa ndipo inatupwa moja kwa moja huko chini. Kwa hiyo hapa ndipo makao ya kila roho mchafu...Mnajua, hiyo ni kweli: upotovu, walawiti, wanawake watovu wa uadilifu.

¹⁹⁶ Angalieni tu kile kilichoanza hapo mwanzo; angalieni katika siku za mwisho kile kilichotukia. Hii hapa papa hapa, imetupwa kwenye Pwani hii ya Magharibi, mitindo ya ulimwengu akiondoka, papa hapa, kutoka Seattle na karibu na hapa, ataenda...Kuna Paris huko nje, wakifanya yasiyofaa, wanawake wao walio uchi, na kila kitu; halafu kuninii...tulikuwa tukienda kule kuchukua mitindo yetu, sasa wanakuja hapa. Aibu kwa taifa hili linalojiita taifa la Kikristo. Mungu, uturehemu, maombi yangu ni kwamba uwaokoe wanaoweza kuokolewa.

¹⁹⁷ Unaweza kuzungumza na Mungu na unazijali nafsi zilizopotea, njoni huku madhabahuni sasa, hebu tuombe pamoja na watu hawa. Njoni, tunapoimba tena. Watu wote wazuri, ninyi wanaume na wanawake watauwa, ambao kweli mnamwamini Mungu, ondokeni vitini mwenu mje hapa juu, na tuombe. Hebu tupate...Hebu tuwafanye watu hawa wajue ya kwamba tuko hapa kuwasaidia. Tuko—tuko hapa kusimama nyuma ya Neno la Mungu, tuko hapa kusaidia. Hiyo ni kweli.

Nimetangatanga mbali...

¹⁹⁸ Baadhi yenu hapa juu, mnaotaka kushuka, ndugu, njoni moja kwa moja, hilo ni sawa. Watu hawa watakuwa wakihudhuria makanisa yenu, kwa hiyo afadhali mshuke mje hapa chini, mnisaidie.

Naja nyumbani;
 Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
 Sasa, Bwana, naja...

(Saa ngapi...?...) Kadi za maombi kesho saa kumi na mbili. Kila mtu...?...

¹⁹⁹ Sasa, kila mtu, hebu na tusimame kwa miguu yetu sasa. Kila mtu, kote huko nje, tunapowaombea hawa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa na kuinua sauti zetu kwa Mungu.

²⁰⁰ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu kutoa shukrani na sifa kwa ajili ya Mwana wa Mungu. Yeye hunena katika Neno Lake, nasi tunamsikia, Sauti Yake inaita kutoka Mbinguni, nasi tunajua ya kwamba Yeye hudumu yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, jalia nguvu za Mungu zije juu ya watu hawa waliosadikishwa na kuwaokoa na maisha ya dhambi. Tujalie, Bwana.

²⁰¹ Huku kanisa likiomba, Shetani ameshindwa. Yule Malaika alisema, "Kama ninaweza kupata watu kumi katika Sodoma ambao ni wenye haki." Ee Mungu, hawa hapa wamesimama, usiku wa leo, idadi kubwa yao, wamesimama tayari, tunangojea mkutano, Bwana, uamsho wa kumiminwa kwa Roho Mtakatifu, na kuponywa wagonjwa. Tujalie, Mungu wa Milele, kupitia Yesu Kristo, Mwanao.

²⁰² Inueni mikono yenu sasa. Aminini kwamba atafanya hivyo. Wekeaneni mikono, ombeni. Iweni na imani na kuamini, Mungu atalijalia. Amina.

(Hakuna haja...) 

62-0711 Msikieni Yeye
Open Bible Standard Church
Spokane, Washington Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org